# ZAWADI KWA WAKRISTO

MWENYEZI MUNGU NI MMOJA

MUHAMMAD S.A.W. KATIKA BIBLIA

YESU A.S. KATIKA QUR'AN

SHEIKH MUZAFFAR AHMAD DURRANI

# ZAWADI KWA WAKRISTO

**Mwandishi - Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani**

**ISBN 9987-8932-5-2**

© Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania

Chapa ya Kwanza, Septemba 2002 nakala 5,000
Chapa ya Pili, Agosti 2010 nakala 2,000

Kimeenezwa na:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
P. O. Box 376
Dar es Salaam -Tanzania
Tel: 2110473 . Fax: 2121744

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam

# YALIYOMO


Masihi wa Quran ... 5
Isa na Yesu ... 9
Yesu si Mungu ... 11
Sifa za Mungu ... 11
Mungu ni Mmoja ... 15
Yesu ni mwana wa Adamu ... 18
Wana wa Mungu ... 20
Yesu Alioa ... 21
Ukoo wa Yesu ... 25
Yesu Mtume wa Mungu ... 27
Yesu, Mtume kwa Waisraeli ... 28
Yesu alileta upanga ... 31
Lugha ya Yesu ... 33
Wanafunzi wa Yesu ... 34
Mizani ya imani ya Wakristo ... 36
Wahalifu wa Yesu ... 38
Paulo ni mhalifu wa Yesu ... 38
Tabiri za Yesu ... 40
Bwana Yesu hakufa msalabani ... 43
Kafara ya Yesu haisaidii chochote ... 54
Mtume Muhammad s.a.w. katika Biblia ... 57
Mwana mkuu wa Ibrahimu ... 68
Ujaji wa Yesu mara ya Pili ... 71
Kupingana kwa maandiko ya Biblia ... 77
Maongezeko katika Biblia ... 85
Aya za Biblia zilizofutwa ... 90
Biblia inavyowadhalilisha Wanawake ... 91
Marejeo mbalimbali ... 94
Maswali kwa Wakristo ... 103

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Mwenyezi Mungu Amemtuma Seyyidna Ahmad a.s. kwa ajili ya kuhakikisha ukweli wa dini ya Kiislamu na ubora wa Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. Kwa kufikia lengo hili vitabu kadha wa kadha vimechapishwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya katika lugha mbalimbali za ulimwengu.

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania imepata bahati ya kuchapisha vitabu zaidi ya sitini juu ya mada kadhaa katika lugha ya Taifa, Kiswahili.

Mwaka juzi Maulana Muzaffar Ahmad Durrani aliandika kijitabu kimoja kinachoitwa **"Silaha za Mahubiri".** Kijitabu hiki kwa hakika kimekuwa ni silaha inayopatikana katika mfuko wa kila Ahmadiyya.

Hata hivyo ndugu wengi walitoa maoni ya kutaka yatolewe maelezo zaidi ya sehemu ya Biblia ili kupanua uwezo wao wa kuyahubiri yaliyomo katika kijitabu hicho. Kwa kuyajibu maoni hayo Sheikh wetu mpendwa Maulana Muzaffar Ahmad Durrani ameandika kitabu hiki, ambacho pia ni **ZAWADI KWA WAKRISTO**. Tunamshukuru na tunamuombea Maulana kwa kazi hii nzuri, Mwenyezi Mungu ambariki na aweke mwongozo katika kitabu hiki. Amin.

Tunategemea kwamba kitabu hiki kitawasaidia wahubiri wetu na kitawafanya ndugu Wakristo wajue kwamba Masihi, mwenye kuvunja msalaba, ameshafika tayari.

**Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania.**

## MASIHI WA QUR'AN

Bwana Yesu Kristo katika Qur'ani Tukufu ameitwa kwa majina ya MASIHI NA ISA. Mama yeke mzazi alikuwa Bi Mariamu. Qur'an Tukufu inawataja kwa heshima kubwa.

Mwenyezi Mungu alim’bashiria Mariamu kumpa mtoto wa kiume (3:46 na 19:20). Mariamu alishangaa kwamba atapataje mtoto hali hajaguswa na mwanamume yeyote (19:21). Lakini Mwenyezi Mungu alisema kwamba haya ni rahisi kwake na jambo hili limekwisha hukumiwa. (19:22). Bwana Yesu alizaliwa katika siku za kuiva tende. (10:26). Na alianza kuongea mambo mazuri katika umri mdogo. (3:47). Alitumwa kwa Waisraeli tu (3:50 na 61:7). Alipewa elimu ya kitabu na hekima. (5:111 na 3:49). Mwenyezi Mungu aliwafunulia wanafunzi wake kumwamini Bwana Yesu Kristo. (5:112). Mwenyezi Mungu alimpatia hoja zilizo wazi na alimsaidia kwa Roho Mtakatifu.(2:254). Mwenyezi Mungu alimwahidi kwamba “Ewe Isa, kwa yakini Mimi nitakufisha na nitakuinua kwangu, na nitakutakasa na (masingizio) ya wale waliokufuru na nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru mpaka siku ya Kiyama...” (3:56). Mayahudi hawakuweza kumuua Masihi wala hawakuweza kumfisha msalabani. (4:158). Bali Mwenyezi Mungu alimfisha kifo cha kawaida. (5:118). Bw. Yesu Kristo aliwaombea wafuasi wake riziki ya kutosha (5:115). Hiyo ni sababu kwamba wafausi wa Bwana Yesu wamejaaliwa riziki ya kutosha.Yeye alipewa heshima

katika dunia na katika Akhera. (3:46). Mwenyewe amesema kwamba ni mtumishi wa Mungu na Mwenyezi Mungu alimusia kuhusu Sala na kutoa Zaka na kumfanyia wema mama yake. (19:31-32). Na aliwasihi watu wake kwamba Mungu wangu na Mungu wenu ni mmoja. Basi mwabuduni Yeye tu. (43:65). Bila shaka hali ya Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama hali ya Adamu. (3:60).

Bwana Yesu Kristo aliishi maisha safi na alishinda katika jukumu lake. Wanafunzi wake walikuwa wasaidizi wa Mwenyezi Mungu na mifano ya kuigwa. (61:15).

Ndugu wasomaji mmesoma jinsi Qur'an Tukufu inavyomheshimu Nabii Isa a.s. na wahusika wake. Hakuna Mwislamu yeyote ambaye anaweza kuwa Mwislamu bila kumwamini na kumheshimu Bwana Yesu. Ningependa kuwaelezeni zaidi kidogo kumbukumbu za Bwana Yesu Kristo zinazopatikana katika Qur'an Tukufu.

**1. <u>Alikuwa mwenye ukoo mtakatifu</u>**

(Ewe Mariamu) baba yako hakuwa mtu m'baya wala mama yako hakuwa asherati. (19:29).

**2. <u>Mariamu alikuwa mkweli</u>**

a. Na mamake (Masihi) ni mwanamke mkweli, (5:76).
b. (Mariamu) akayasadikisha maneno ya Mola wake, ( 66:13).

**3. <u>Alikuwa mtiifu mbele ya mamake</u>**

Na (Allah Ameniusia) kumfanyia mema mama yangu,

wala Hakunifanya niwe jeuri mwenye bahati mbaya (19:33).

**4. <u>Alikuwa mtakatifu</u>**

Na Tukampa Isa mwana wa Mariamu Ishara zilizo wazi na tukamsaidia na Roho Mtakatifu (maneno matakatifu) (2:88).

**5. <u>Alikuwa mtu wa Mungu</u>**

Akasema mimi ni mtumishi wa Mwenyezi Mungu. Amenipa kitabu na Amenifanya Nabii na Amenifanya m'barikiwa popote nilipo, na Ameniusia Sala na Zaka maadam ningali hai (19:31-32).

**6. <u>Alikuwa mfano mwema</u>**

Na Tukamfanya methali (mfano) kwa wana wa Israili. (43:60).

**7. <u>Alikuwa mtu wa amani.</u>**

Na amani iko juu yangu siku niliyozaliwa na siku nitakayokufa na siku nitakayo fufuliwa kuwa hai. (19:34).

**8. <u>Alikuwa neno la Mungu</u>**

Masihi Isa bin Mariam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno lake tu Alilompelekea Mariamu. (4:172)

9. **<u>Mtume wa kweli anapewa habari za ghaibu</u>**

(Mwenyezi Mungu) Yu mjuzi wa siri, wala hamdhihirishii yeyote siri yake, isipokuwa Mtume aliyemridhia. ( 72:27-28).

Hivyo Masihi Isa a.s. alipewa habari za ghaibu.

**10. <u>Aliwasadikisha Mitume wa zamani na alitabiri Mtume ajaye</u>**

(Isa a.s. akasema) nisadikishaye yaliyo mbele yangu katika Taurati na kutoa habari njema ya Mtume atakayekuja nyuma yangu jina lake ni Ahmad. (61:7).

**11. <u>Alizaliwa bila baba</u>**

A. (Mariamu) akasema Mola wangu, nitapataje mtoto na hali mtu yeyote hakunigusa? (Mungu) Akasema: Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Hutenda anavyopenda. (3:48, 19:21).

B. Masihi alikuwa mwana wa Mariamu. (4:172, 5:76).

Islam haijengi ukuta wa husuda na bughudha baina ya Waislamu na Wakristo. Bali inawakaribisha katika mambo ya kheri na ya kujumuika. Qur'an Tukufu imesema kwamba: “Enyi watu wa kitabu, njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na baina yenu, ya kwamba tusimwabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote.” (3:65). Vilevile Qur'an Tukufu inawasifu Wakristo na inawapongeza. Imesema kwamba: “....na utawaona walio karibu zaidi kwa urafiki na waaminio ni wale wanaosema ya kuwa sisi ni Wakristo. Hayo ni kwa sababu wako miongoni mwao makasisi na maruhubani, na kwa sababu wao hawatakabari.” (5:83).

Kwa njia hii Qur’an Tukufu inajenga urafiki na Wakristo. Kwahiyo ninawakaribisheni ndugu Wakristo

katika dini ya Mwenyezi Mungu, ili tuwe kitu kimoja na tujenge umoja na tupate amani. Na hii ni zawadi kwa Wakristo. Karibuni sana.

Lakini baadhi ya Mapadri na Wachungaji wanayo shauku kubwa kuwatenganisha Waislamu na Wakristo. Wanafundisha husuda na bughudha katika jamii. Wanafitinisha mtoto kwa mzazi, ndugu kwa ndugu. Hata wanajaribu kuthibitisha kwamba Waislamu na Wakristo ni maadui, ilhali Qur'an Tukufu inawaita marafiki.

Wengine wanatofautisha kiasi hiki kwamba, wanasema Yesu wa Biblia na Isa wa Qur'an ni watu wawili tofauti, ili usibaki uhusiano baina ya Waislamu na Wakristo. Wengine wanatumia lugha chafu kwa ajili ya dini ya Islam na kwa ajili ya viongozi wake. Siku hizi mifano yake inapatikana nchini katika magazeti ya Kikristo kama vile *"Msema Kweli"* na *"Nyakati."*

Sasa kwa ajili ya kuwapatia akili kidogo nimelazimika kuwaonesha hawa wapinzani wa dini ya Islam na viongozi wake. Kila somo litatoka kutoka Biblia tu.

# ISA NA YESU

***(Kutoka maandishi ya Sayyidna Ahmad a.s.)***

Tunamwamini na tunamheshimu Masihi wa kweli na mtakatifu ambaye hakudai kuwa mungu au mwana wa Mungu na alitabiri ujaji wa Mtume Muhammad s.a.w. (Fathe-e-Masih uk. 13).

Ni jukumu langu kuthibitisha kwamba Isa a.s. alikuwa nabii mkweli na Mtakatifu wa Mwenyezi Mungu (Ayyam-us-Sulh uk. 2).

Mimi ni mfano wa Isa a.s. kwa hiyo siwezi kumwita mbaya. (Tabligh-e- Risalat uk. 70).
Hatumtambui Yesu ambaye alidai kuwa mungu na akawaita wa kabla yake kuwa wezi na wa baadaye waongo. (Anjam-e-Atham uk. 9).

Mapadre kwa kumtusi Mpendwa wetu Mtume Muhammad s.a.w. wametulazimisha kueleza hali kidogo ya Yesu na vitendo vyake (sawa na alivyoelezwa katika Biblia). Kama mapadre watubu na waahidi kwamba hawatamtusi Mtume Muhammad s.a.w., sisi pia hatutadhihirisha hali na siri zao waila litakuwa jiwe kwa jiwe. (Anjam-e-Atham uk. 8).

## YESU SI MUNGU:
## <u>KWA SABABU HANA SIFA ZA MUNGU</u>

Mwenyezi Mungu Anazo sifa zifuatazo ambazo Yesu hanazo hata sifa moja wapo. Mwenyezi Mungu ndiye muumba wetu ambaye ni mmoja. Anajulikana na anatambulikana kwa sifa zake. Biblia inatuelezea sifa hizo. Hapa chini nitaeleza baadhi ya sifa za Mwenyezi Mungu zinazotajwa katika Biblia. Vilevile nitaeleza kwamba Bwana Yesu Kristo hana hata sifa moja sawa na Biblia.

### 1. <u>MUNGU HAJARIBIBIWI</u>

Biblia inasema kwamba: "Mtu ajaribiwapo, asiseme, ninajaribiwa na Mungu; maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala mwenyewe hamjaribu mtu," (Yakobo 1:13). Sasa tuone hali ya Bwana Yesu Kristo kwamba yeye anayo sifa hii au ni kinyume chake. Biblia inasema kwamba: " Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi," (Mathayo 4:1). Mungu hajaribiwi lakini Yesu alijaribiwa na Iblisi, kwahiyo hawezi kuwa mungu, kwa sababu ya kukosa sifa hii ya Mungu.

### 2. <u>MUNGU HAFI</u>

Mwenyezi Mungu ni hai ambaye anadumu milele na hatakufa. Akili inakubali kwamba Mungu ni yule ambaye anao uzima wa milele kama Biblia inavyosema kwamba: "Mimi naweka amri, ya kwamba katika mamlaka yote, ya ufalme wangu watu

watetemeke na kuanguka mbele za Mungu wa Danieli; maana yeye ndiye Mungu aliye hai, adumuye milele, na ufalme wake ni ufalme usioharibika, mamlaka yake itadumu hata mwisho." (Danieli 6:26).

Sasa tuone kwamba je, Bwana Yesu anayo sifa hii ya Mungu ya kuwa hai milele bila kifo. Biblia inaeleza kwamba Bwana Yesu hana sifa hii: "Naye Yesu akisha kupaza sauti tena kwa nguvu akaitoa roho yake." (Mathayo 27:50). Hivyo mtu ambaye alifariki hawezi kuwa Mungu. Wakristo wanaamini kwamba Bwana Yesu alifariki kifo cha laana lakini sisi Waislamu tunaamini kwamba Yesu hakufa kifo cha laana bali alisaidiwa na Mwenyezi Mungu na aliweza kuhamia nchi za Mashariki, aliishi kule maisha ya mafanikio. Alipokelewa na kondoo waliopotea wa nyumba ya ISRAELI, na alifariki kifo cha kawaida katika uzee wake wa umri wa miaka 120. Kaburi lake linapatikana katika mtaa wa Khan'yar mji wa Srinagar, jimbo la Kashmir, nchini India. Kwa maelezo zaidi soma vitabu vifuatavyo. "Yesu Katika India" na "Yesu kafia Wapi?"

Hata hivyo, pamoja na tofauti hizo za uelewa bado Wakristo na Waislamu wanakubaliana kwamba Yesu alikufa, na hivyo hawezi akawa Mungu kwa kukosa sifa ya uhai wa milele bila ya kufa.

## 3. MUNGU ANAJUA KILA KITU

Ni sifa ya Mwenyezi Mungu kujua kila kitu cha dhahiri na cha siri. Kitu chochote hakiwezi kufichika kwake. Kama Biblia inavyosema kwamba: "Basi usikie huko mbinguni, makao yako, ukasamehe, ukampe kila mtu kwa kadri ya njia zake; wewe ujuaye moyo wake;

(maana wewe peke yako ndiwe uijuaye mioyo ya wanadamu wote.” (1Wafalme 8:39).

Sasa tuone kiwango cha Bwana Yesu cha kujua mambo. Biblia inasema kwamba: “Hata asubuhi alipokuwa akienda mjini, aliona njaa. Akaona mtini mmoja kando ya njia, akauendea, asione kitu juu yake ila majani tu; akauambia, yasipatikane matunda kwako tangu leo hata milele. Mtini ukanyauka mara.” (Mathayo 21:18-19).

Mtu ambaye hajui kwamba msimu huu mti fulani haupatikani matunda ilhali hata watoto wadogo wanajua misimu ya matunda mbalimbali, hawezi kuwa Mungu.

Tena aya hii inaonesha tabia ya Bwana Yesu kwamba mwenyewe alikosea kujua msimu wa matunda ya mtini na kisha akaulaani mti bure.

Pia Bw. Yesu anakiri mwenyewe kwamba hajui chochote kuhusu habari za saa ile (Mathayo 24:36).

## 4. <u>MUNGU HACHOKI</u>

Mwenyezi Mungu hana kasoro ya udhaifu wowote. Sifa zote njema zinamhusu yeye. Biblia inasema kwamba: Je, wewe hukujua? hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana muumba miisho ya dunia, hasinzii wala hachoki, akili zake hazichunguziki.” (Isaya 40:28).

Sasa tuone hali ya Yesu. Je, yeye anayo sifa hii ya Mungu? Kama hana, basi hawezi kuwa Mungu. Biblia inasema: “Na hapo palikuwa na kisima cha Yakobo, Basi Yesu kwa sababu amechoka kwa safari yake, akaketi vivi hivi kisimani. Nayo yapata saa sita.” (Yohana 4:6). Basi mwenye kuchoka hawezi kuwa Mungu.

## 5. MUNGU HAUWAWI

Mwenyezi Mungu ndiye mwenye mamlaka na nguvu zote na anao uwezo kamili, hawezi kushindwa mbele ya yeyote: “Watakushusha hata shimoni; nawe utakufa kifo chao waliouawa kati ya bahari. Je, utazidi kusema mbele yake huyo akuuaye, Mimi ni Mungu? Lakini u mwanadamu, wala si Mungu, mkononi mwake akutiaye jeraha.” (Ezekieli 28:8-9). Mwanadamu anauawa na bwana Yesu anayo sifa hii sawa na Biblia. “Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu, ambaye ninyi mlimuuwa mkimtundika katika mti.” (Matendo 5:30).

Basi mtu ambaye anatundikwa na anauawa hawezi kuwa Mungu. Bali ataitwa mtu dhaifu. Sisi Waislamu hatuamini kabisa kwamba Bwana Yesu aliuawa. Maadui wake hawakuweza kumuuwa bali yeye alisalimika na alihamia nchi za mashariki sawa na sunna za manabii.

## 6. MUNGU HASINZII WALA HALALI

Mwenyezi Mungu ni mwenye uwezo wa aina zote ambaye hahitaji kupumzika wala kusinzia. Biblia inasema kwamba: “Naam, hatasinzia wala hatalala usingizi, yeye aliye mlinzi wa Israeli.” (Zaburi 121:4).

Sasa Mungu hahitaji kusinzia wala kulala lakini Bwana Yesu alikuwa akilala sana. Kwahiyo hawezi kuwa Mungu. Biblia inasema kwamba: Ilitokea dhoruba kuu ya upepo, mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji. Naye mwenyewe alikuwapo katika shetri, amelala juu ya mto, wakamwamsha, wakamwambia, mwalimu, si kitu kwako kama tunaangamia? (Marko 4:37-38; Mathayo 8:23-25).

## YESU SI MUNGU:
## <u>KWA SABABU MUNGU NI MMOJA TU</u>

Baadhi ya Wakristo wanatafuta sababu na udhuru wa kumfanya Yesu kuwa Mungu. Kwa mfano husema kwamba Yesu ni Mungu au mwana wa Mungu au Yesu ni Mungu mdogo au Yesu ni nafsi moja ya Mungu. Mambo haya yote ni kufuru tupu iliyovuka mipaka. Kwa sababu sawa na Biblia Mungu ni mmoja tu. Hakuna Mungu mdogo wala Mungu mwana.

Biblia inasema:-

1. Wewe naam, wewe peke yako ndiye Mungu wa falme zote za dunia; wewe ndiwe uliyeziumba mbingu na nchi. (2 Wafalme 19:15).
2. Kwa kuwa ndiwe mkuu, wewe ndiwe mfanya miujiza, ndiwe Mungu peke yako. (Zaburi 86:10).
3 Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma, (Yohana 17:3).

Sasa wakati Mungu wa pekee ni mmoja, hivyo Mungu zaidi ya mmoja ni wa uwongo.

4. Mwawezaje kuamini ninyi, mnaopokeana utukufu ninyi kwa ninyi, na utukufu ule utokao kwa Mungu aliye wa pekee hamwutafuti? (Yohana 5:44).
5. ...Hakuna Mungu ila mmoja tu. Kwa maana ijapokuwa wako waitwao miungu, ama mbinguni au duniani; kama vile walivyoko miungu mingi na mabwana wengi. Lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu. aliye baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake. (1 Wakorintho 8:4-6). Sawa na aya hizi hakuna Mungu

ila mmoja tu. Ingawa miungu wa bandia wanatajwa tajwa mbinguni na ardhini. Basi sasa ambaye anaamini mungu minghairi ya Mwenyezi Mungu anatoka katika imani na anaingia katika ushirikina kwa sababu ya kuwaita miungu zaidi ya mmoja ambaye ni wa kweli na wa pekee.

6. ..Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu. (Marko 2:7). Aya hii inathibitisha kwamba mwenye kufuta na kuondoa dhambi ni mmoja tu ambaye ni Mungu. Yaani hakuna mungu wa pili wala wa tatu wala mwenye kufuta dhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Siyo aya hizo tu, bali tunaposoma Biblia tunakuta msululu wa aya kadhaa ambazo zinataja umoja wa Mungu. Kwa mfano: Kumbukumbu 4:39, 6:4; Nehemia 9:9; Isaya 43:10-11; 44:6-8, 44:5. 45:21-22, 46:9; Marko 12:32; Luka 18:19; Mathayo 4:10; Warumi 3:30; Timotheo 1:17, 2:5. Hakuna aya hata moja inayosema kwamba Yesu ni Mungu.

## YESU SI MUNGU: KWA SABABU MUNGU YUPO NDANI NA PAMOJA NA WENGINE PIA

Baadhi ya Wakristo wanadhani kwamba Yesu ni Mungu kwa sababu ya baadhi ya maandiko ya Biblia yanayosema kwamba Yesu yupo pamoja na Mungu, bali Mungu yupo ndani ya Yesu na Yesu yupo ndani ya Mungu.

Maandishi ya aina hii yote hayamaanishi kwamba

Yesu ni Mungu bali yanaonesha kwamba Mungu na Yesu ni tofauti tofauti wala siyo kitu kimoja. Vile vile Biblia haisemi kwamba mtu ambaye anatajwa kuwa ndani ya Mungu au Mungu yumo ndani yake ni mungu. Kinyume chake Biblia inatutajia watu kadhaa wale ambao wako pamoja na Mungu na Mungu yupo ndani yao na hawa wapo ndani ya Mungu. Tena hakuna Padre yeyote ambaye anawaita watu hawa miungu.

Wakati watu wengine kwa sifa zile zile hawaitwi miungu, kwa msingi na kwa uzuri gani, Yesu aitwe Mungu? Biblia inasema kwamba:

1. “Wote wawe na umoja, kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; Hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujuwe ya kuwa ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi. (Yohana 17:21-23).
2. Mungu mmoja, naye ni baba wa wote aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote. (Waefeso 4:6)
3. Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya baba yangu, nanyi ndani yangu, mimi ndani yenu. (Yohana 14:20).
4. Nabii Suleimani anasema kwamba: Mimi nilikuwepo pamoja na Mungu hata kabla ya kuumbwa ardhi na mbingu, (Mithali 8:22-30).
5. ....Lakini enenda kwa ndugu zangu ukawambie, ninapaa kwenda kwa baba yangu naye ni baba yenu,

kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu. (Yohana 20:17).

6. Kama Wakristo waseme kwamba Yesu ni mungu kwa sababu alizaliwa bila baba. Najibu kwamba aya gani inasema kuwa azaliwaye bila baba ni Mungu? Na malaki ya wadudu wanaozaliwa bila baba watakuwa na uhusiano gani na Bwana Yesu?

Katika Biblia mfano mzuri zaidi kuliko Yesu unapatikana kwamba: Melkizedeki mfalme wa Salem hana wazazi, hana mwanzo na mwisho, (Waebrania 7:3). Sasa kama Yesu anaitwa mungu kwa sababu ya kuzaliwa bila baba, Melkezedeki atakuwa mungu mkuu kwa sababu hana wazazi, hana mwanzo hana mwisho. Wakristo wanasemaje hapa?

## 4 YESU SI MUNGU:
## KWA SABABU NI MWANA ADAMU

Hakuna aya yoyote katika Biblia inayosema kwamba Yesu ni mungu, kinyume kabisa na baadhi ya Wakristo wanaoamini kwamba Yesu ni mungu. Tunaposoma Biblia tunakuta aya kadhaa zinazoeleza kwamba Yesu ni mwana wa Adamu. Basi mwana wa Adamu hawezi kuwa mungu wala mwana wa Mungu.

Biblia inasema:

1. Mwana wa Adamu alikuja akila na kunywa, wakasema mlafi huyu na mlevi. (Mathayo 11:19).
2. Kwani kama vile Yona alivyokuwa mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo, Mwana wa

Adamu atakavyokuwa kwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi. (Mathayo 12:40).

3. Yesu akamwambia, mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota, lakini mwana wa Adamu hana pa kulaza kichwa chake. (Mathayo 8: 20). Tunaposoma Biblia tunakuta mara nyingi sana Yesu anaitwa Mwana wa Adamu. Kwa mfano: Mathayo 8:20, 9:6, 12:40, 14:28, 16:27, 17:22, 24:30 na 26:45. Marko 2:10, 9:31 na 14:21-40. Luka 9:44. Yohana 5:27 na Matendo 7:56.

Kama Mwana wa Kondoo ni kondoo - Mwana wa mbuzi huwa ni mbuzi vile vile Mwana wa Adamu ni binadamu. Haieleweki ni kwa sheria na kanuni gani Mwana wa Adamu anapachikwe jina la Mungu au Mwana wa Mungu?

4. Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo, Mwana wa Daudi, Mwana wa Ibrahim. (Mathayo 1:1).

## 5. YESU SI MUNGU: KWA SABABU SIYO MWANA PEKE YAKE

Baadhi ya Wakristo wanadai kwamba Yesu ni Mungu kwa sababu kuna sababu ya kuitwa Mwana wa Mungu. Kama mwana wa Mungu anaweza kuwa Mungu basi tuone kati ya hawa wana wa Mungu na kwa nini wote wasiwe miungu? Na kwa nini Mwana wa Kwanza asiwe Mungu?

## WANA WA MUNGU

Biblia inasema kwamba: 1. Bwana asema hivi, Israeli ni mwanangu mimi, mzaliwa wa kwanza wangu. (Kutoka 4:22).

2. Daudi ni mwana wa Mungu, yeye pia ni mwana wa kwanza. (Zaburi 89: 26-27).

3. ....maana mimi ni baba wa Israeli na Efraim (Ibrahim) ni mzaliwa wa kwanza wangu. (Yeremia 31:9). Hawa wana wa Mungu wote, kila mmoja wao ni mzaliwa wa kwanza kwa Mungu. Kwanza itakuwaje watoto wote watatu wawe wazaliwa wa kwanza kwa Mungu. Pili kwa nini hawa wazaliwa wa kwanza wasiitwe miungu? Na kama hawa watatu wakubwa hawawezi kuwa miungu wala hawaabudiwi, basi mtoto mdogo Yesu pia hana haki yoyote ya kuitwa Mungu wala hana haki ya kuabudiwa.

4. Suleimani ni Mwana wa Mungu. (Mambo ya Nyakati 22:9-10).

5. Wapatanishao wameitwa Wana wa Mungu. (Mathayo 5:9). Oo! siyo tu bali katika Biblia baadhi ya watu wameitwa miungu. Tena hakuna Mkristo ambaye anawaita miungu wala hawaabudiwi. Kama Biblia inavyosema kwamba:

A. Yesu akawajibu, Je! haikuandikwa katika Torati yenu ya kwamba, mimi nimesema, ndinyi miungu? (Yohana 10:34).

B. Bwana akamwambia Musa angalia, nimekufanya wewe kuwa kama mungu kwa Farao na huyo ndugu yako Harun atakuwa Nabii wako. (Kutoka 7:1).

## 6. YESU SI MUNGU: KWA SABABU WENGINE PIA WALIFUFUA WAFU

Wakristo wengine wanasema kwamba Yesu ni Mungu kwa sababu ya kufufua wafu. Nauliza imeandikwa wapi kwamba mtu ambaye anafufua wafu ni Mungu? Ya pili wale wengine ambao walifufua wafu pia wanaitwa miungu? Biblia inaeleza kwamba watu wengine pia walifufua wafu na hawaitwi miungu. Ikiwa kwa sababu ya kufufua wafu hawaitwi miungu, basi Yesu pia hana haki yoyote ya kuitwa Mungu. Biblia inasema: 1. Elisha alifufua mtoto aliyefariki. (2 Wafalme 4:35). (2) Maiti alifufuka kwa kuguswa na mifupa ya Elisha. (2 Wafalme 13:21). 3. Ezekiel alifufua jeshi kubwa. (Ezekiel 37:10).

## 7. YESU SI MUNGU: KWA SABABU ALIOA

Wakristo wanasema kwamba Yesu ni Mungu na ndiyo sababu hakuoa katika maisha yake. Tunauliza ni aya gani ya Biblia inayosema kwamba mtu ambaye haoi anaitwa Mungu? Na watu wale ambao hawakujaaliwa kuoa, je, ni miungu ya Wakristo?

Qur'an Tukufu inaeleza kwa jumla kwamba mitume walioa na wakajaaliwa watoto. “Na bila shaka Tuliwatuma mitume kabla yako, na Tukawapa wake na watoto. (Qur'an 13:19).

**MKE WA YESU**

Biblia inasema kwamba Bwana Yesu Kristo alikuwa akipatikana na mwanamke mmoja aitwaye Mariam Magdalena. Yeye alikuwa karibu sana na Yesu. Vitendo vyao vinaonesha kwamba, walikuwa mume na mke au marafiki wapenzi. Sisi hatuamini kwamba nabii anafanya urafiki na mwanamke na kumpangusa miguu yake kwa kichwa na kum'busu, bali yeye alikuwa mke wake. Basi tusome Biblia kisha tuone kwamba huyo alikuwa nani?:

1. "Na tazama, mwanamke mmoja wa mji ule, aliyekuwa mwenye dhambi, alipopata habari ya kuwa ameketi chakulani katika nyumba ya yule Farisayo, alileta chupa ya marhamu. Akasimama nyuma karibu na miguu yake, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake, akiibusu-busu miguu yake na kupaka yale marhamu. Basi yule Mfarisayo aliyemwalika alipoona vile, alisema moyoni mwake. Mtu huyu kama angekuwa nabii angemtambua mwanamke huyu amgusaye, ni nani, na ni wa namna gani ya kwamba ni mwenye dhambi. (Luka 7:37-38).

2. "Basi mtu mmoja alikuwa hawezi Lazaro wa Bethana, mwenyeji wa mji wa Mariamu, dada yake. Ndiye Mariam yule aliyempaka Bwana marhamu, akamfuta miguu kwa nywele zake, ambaye Lazaro nduguye alikuwa hawezi (Yohana 11:1-2).

3. "Basi Mariam akatwaa ratili ya marhamu ya nardo safi yenye thamani nyingi, akimpaka Yesu miguu, akamfuta miguu kwa nywele zake.'' (Yohana 12:3).

4. "Akamgeukia yule mwanamke, akamwambia

Simoni, wamuona mwanamke huyu? niliingia nyumbani kwako, hukunipa maji kwa miguu yangu, bali huyu amenidondoshea machozi miguu yangu; na kuipangusa kwa nywele zake. Wewe hukunibusu; lakini huyu tangu nilipoingia hakuacha kunibusu sana miguu yangu. Hukunipaka kichwa changu mafuta; bali huyu amenipaka kichwa changu mafuta'' (Luka 7:44-46).

5. "Basi Mariamu pale alipokuwapo Yesu, na kumuona, alianguka miguuni pake, akamwambia Bwana, kama ungalikuwepo hapa, ndugu yangu hangali kufa. Basi Yesu alipomuona analia na wale Wayahudi aliyofuatana nao wanalia, aliugua rohoni, akafadhaika roho yake akasema mmemweka wapi? Wakamwambia, Bwana, njoo utazame. Yesu akalia machozi.'' (Yohana11:32-35).

6. "Biblia inaeleza habari ya arusi moja, iliyofanyika huko Kana ya Galilaya. Imeandikwa: "Na siku ya tatu palikuwa na arusi huko Kana, mji wa Galilaya; naye mama yake Yesu alikuwapo, Yesu naye alikuwa amealikwa arusini pamoja na wanafunzi wake. Hata divai ilipowatindikia, mamaye Yesu akamwambia, Hawana divai. Yesu akamwambia, Mama, tuna nini mimi nawe? Saa yangu haijawadia. Mamaye akawaambia watumishi, lolote atakalowaambia, fanyeni. Basi kulikuwako huko mabalasi sita ya mawe, nayo yamewekwa huko kwa desturi ya Wayahudi ya kutawadha, kila moja lapata kadiri ya nzio mbili tatu. Yesu akawaambia, jalizeni mabalasi maji. Nao wakayajaza hata juu. Akawambia, sasa tekeni, mkampelekee mkuu wa meza. Wakapeleka. Naye

mkuu wa meza alipoyaonja yale maji yaliyopata kuwa divai, (wala asijue ilikotoka, lakini watumishi walijua, wale walioyateka yale maji), Yule mkuu wa meza alimwita Bwana arusi, akamwambia, kila mtu kwanza huandaa divai iliyo njema; hata watu wakiisha kunywa sana ndipo huleta iliyo dhaifu; wewe umeiweka divai iliyo njema hata sasa." [Yohana 2:1-10].

Katika aya hizi mambo yafuatayo yanathibitisha kwamba arusi ile ilikuwa ya Bwana Yesu Kristo.

(A) Bwana Yesu, mama yake na wanafunzi wake walikuwepo huko. Kualikwa katika arusi ya mtu mwingine haingewezekana. Kwa sababu hawakuwa na uhusiano mzuri na watu wengine, ila waalikwa wote. Basi arusi ilikuwa ya Yesu mwenyewe.

(B) Wakati divai ya arusi ilipokwisha, Mariamu mama yake Yesu, alishituka na alihangaika sana, na mara moja alikwenda kwa Bwana Yesu kumwambia afanye chochote sasa, maana itakuwa fedheha mbele ya wageni. Mahangaiko ya Bi Mariamu yanaonesha kwamba yeye hakuwa mgeni bali alikuwa mwenyeji na msimamizi wa arusi ya mwanawe Yesu. Waila wageni hawatishiki kwa kupungua au kwisha chakula.

(C) Wakati Bwana Yesu aliambiwa apange mpango wa kuongeza divai ya arusi, alimwambia mama yake kwamba leo mimi ni bwana arusi, hivyo siwezi kuhangaika. Kwa sababu ya kukaa juu ya kiti cha Bwana arusi, saa yangu haijawadia.

(D) Bi Mariam aliwaita wanafunzi kumsaidia Yesu kupanga mpango wa divai, wote walishughulika kufanya kazi ile. Hiyo inaonesha kwamba arusi ilikuwa

ya Bwana Yesu na wanafunzi wake walikuwa wakimsaidia katika shughuli za arusi. Maana hawakuwahi kufanya kitu kama hiki kabla.

(E) Mkuu wa meza alikuwa mtu mwingine. Kama arusi alikuwa siyo Yesu basi yeye angekuwa mkuu wa meza kulingana na heshima yake. Lakini kama Yesu alikuwa bwana arusi basi mwingine anaweza kuwa mkuu wa meza.

(F) Yule mkuu wa meza alimwita bwana arusi na kumpongeza kwa kutengeneza divai nzuri. Kwavile bwana Yesu ndiye aliyetengeneza divai basi ni yeye pia aliyekuwa bwana arusi.

Basi arusi ya Kana ya Galilaya ilikuwa ni arusi ya Bwana Yesu.

Je, mtu aliyeendelea kufanya mapenzi na mwanamke au aliyeoa anaweza kuwa mungu?

## UKOO WA YESU

Sisi Waislamu tunaamini kwamba Bwana Yesu a.s. alikuwa Nabii wa Mungu. Na manabii wote ni watukufu na wapendwa wa Mwenyezi Mungu. Wanatoka kutoka koo takatifu. Kuhusu ukoo wa Bwana Yesu Kristo Masihi Mwana wa Mariamu a.s. Qur'an Tukufu inaeleza kwamba:

A. Masihi bin Mariamu siye ila ni Mtume tu, bila shaka mitume wote wamekwisha fariki kabla yake, na mama yake ni mwanamke mkweli. (Qur'an 5:76).

B. (Ewe Mariam) baba yako hakuwa mtu m’baya wala mama yako hakuwa asherati. (Qur'an 19:29).

Kwa hiyo sawa na mafundisho ya dini ya Kiislamu tunamheshimu Nabii Isa a.s. (Yesu Kristo) na vile vile wazee wake.

Sisi tunashangaa sana wakati tunaposoma Biblia, tunaona Biblia inamfedhehesha Yesu Kristo vibaya sana. Licha ya kuwa Mtume wa Mungu sawa na Biblia, Bwana Yesu haonekani hata mtu mwenye ukoo safi, bali tunalazimika kumtafautisha Isa a.s. na Yesu. Biblia inasema kwamba:

1. Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi mwana wa Ibrahim. (Mathayo 1:1).
2. Salmoni akamzaa Boazi kwa Rahabu. (Mathayo 1:5) Rahabu alikuwa kahaba (Yoshua 2:1).
3. Yuda alimzaa Peresi na Zera kwa Tamari (Mathayo 1:3). Tamari alikuwa kahaba na mzinifu. (Mwanzo 38:13-18).
4. Daudi alimzaa Sulemani kwa yule mke wa URIA (Mathayo 1:6). Beth Sheba mkewe URIA alipata mimba ya zinaa. (2 Samuel 11:2-5).

Hawa mabibi wote wa Yesu Kristo walikuwa makahaba na wazinifu. Lakini sisi hatukubaliani na Biblia bali tunaona kwamba ni taka taka zilizoongezwa katika Biblia. Na kama Wakristo wanang'ang'ania usahihi wa Biblia, basi wajuwe kwamba Biblia inasema: "Mwana wa haramu asiingie katika mkutano wa Bwana; hata kizazi cha kumi asiingie aliye wake katika mkutano wa Bwana. (Kumb. la Torati 23:2).

Enyi ndugu Wakristo! Kama mnaona kwamba Biblia bado ni sahihi basi mjue kwamba Yesu ni kizazi cha

wazinifu, hawezi kuingia katika mkutano wa Mungu. Kama hawezi hata kuingia katika mkutano wa Mungu, ninyi mnamtegemea nini? Karibuni, Muhammad s.a.w. mfano wa Musa anawakaribisheni kwa mikono miwili. Kama mnaona kwamba Yesu Kristo ni mtakatifu lakini Biblia imechafuka kwa mikono ya waandishi, pia karibuni katika dini ya Kiislamu. Qur'an kitabu cha Mungu kitawatoshelezeni. Maana sasa hakuna njia ya kusalimika isipokuwa katika dini ya Kiislam. Kwahiyo karibuni sana.

## YESU KRISTO NI MTUME WA MUNGU

Sisi Waislamu tunaamini, sawa na Qur'an Tukufu kwamba Bwana Yesu Kristo (Isa bin Mariamu) alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Kama Mwenyezi Mungu alivyosema katika Qur'an Tukufu (4:172, 5:76, 61:7).

Ndugu Wakristo wanampandisha daraja la juu kuwa mwana wa Mungu na mungu. Bado hatujaelewa ni kwa misingi gani Wakristo wanampendelea hivi ambapo Biblia inaeleza vizuri sana kwamba: Akajibu, akasema sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. (Mathayo 15:24).

2. Na uzima wa milele ndiyo huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma. (Yohana 17:3).

3. ... bali yeye ndiye aliyenituma. (Yohana 8:42).

4. ... Bali baba aliyenipeleka. (Yohana 14:24).

5. ... Wewe ndiye uliyenituma.
(Yohana 17:8-14, 21-22)

6. Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe, kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo. Na hukumu yangu ni ya haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka. (Yohana 5:30, 6:38, 4:36). Isitoshe siyo hayo tu, bali Injili zote zimejaa aya zinazoeleza kwamba Yesu ni Mtume tu. Kwa faida ya wasomaji wetu ninataja hapa aya chache tu. (Mathayo 21:46, 21:11, 9:37. Marko 9:35, Luka 4:43, 24:19. Yohana 13:20, 12:44-50, 7:16-17, 6:44, 7:28-33, 8:16-18, 26-29, 9:4,19:17, 6:14, 15:22, 16:5,17:21-25, 4:19-24-44.

## YESU ALITUMWA KWA WANA WA ISRAELI TU

Hapa juu mmekwisha soma tayari kwamba Yesu hakuwa Mungu wala mwana wa Mungu bali alikuwa Mtume wa Mungu tu. Yeye hakupewa ujumbe wa utume kwa ajili ya watu wote wa kabila zote. Bali yeye alikuwa Mtume kwa ajili ya wana wa Israeli tu. Mwenyewe alijua mipaka ya utume wake. Kwahiyo alisema:

1. Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. (Mathayo 15:24).
2. Wakati mwanamke mmoja asiyekuwa mwana wa Israeli alipokuja kwa Yesu Kristo kuomba baraka zake, Yesu akakataa na zaidi ya kukataa aliwatusi wasiokuwa Waisraeli. “Akasema si vyema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia m’mbwa.” (Mathayo 15:26, Marko 7:27).
3. Hao thenashara (kumi na mbili) Yesu aliwatuma, akawaagiza, akisema, katika njia ya mataifa msiende,

wala katika mji wowote wa Wasamaria msiingie. Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. (Mathayo 10:5-6).

4. Baadhi ya Wakristo wanadhani kwamba wakati Waisraeli wote wamefikishiwa ujumbe, kisha makabila mengine pia yahubiriwe. Lakini dhana hii si sahihi bali ni kinyume cha mafundisho ya Bwana Yesu. Yeye amesema kwamba: “Lakini watakapo wafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine; kwa maana ni kweli nawambia, hamtaimaliza miji ya Israeli hata ajapo mwana wa Adamu. (Mathayo 10:23).

5. Bwana Petro mwanafunzi wa Yesu Kristo aliwahubiri wasiokuwa Waisraeli. Wanafunzi wengine, baada ya kupata habari hii walimpinga Bwana Petro kwa kosa lake. Biblia inasema kwamba: “Basi mitume na ndugu waliokuwako katika Uyahudi wakapata habari ya kwamba watu wa mataifa nao wamelipokea neno la Mungu. Na Petro alipopanda kwenda Yerusalemu, wale walio wa tohara wakashindana naye, wakisema, uliingia kwa watu wasiotahiriwa ukala nao. “ (Matendo 11:1-3).

6. Aya za Biblia zifuatazo zinaeleza kwamba Bwana Yesu alikuwa mfalme na mtawala wa Mayahudi. (Mathayo 2:6, 27:29, 27:42, Yohana 1:49.

7. Bwana Paulo ambaye ni mpinzani na mhalifu *(anti Christ)* wa Bwana Yesu, baada ya kuchukia alianza mahubiri nje ya Wasiraeli. Biblia inasema kwamba: “Hata Sila na Timotheo walipoteremka kutoka Makedonia, Paulo akasongwa sana na bila neno, aliwashuhudia Wayahudi ya kwamba Yesu ni Kristo walipopingana naye na kumtukana Mungu,

akakung'uta mavazi yake, akawaambia, damu yenu na iwe juu ya vichwa vyenu, mimi ni safi; tangu sasa ninakwenda kwa watu wa mataifa. (Matendo 18:5-6).

Baadhi ya Wakristo wanayo shauku ya kugonganisha aya za Biblia. wanasema kwamba Bwana Yesu aliagiza kwamba “Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi.” (Mathayo 28:19).

1. Najibu kwamba aya hii inapinga maagizo yote ya Bwana Yesu yaliyotajwa juu. Kwahiyo haiwezi kuwa agizo la Yesu wala aya ya Injili.

2. Ya pili aya hii imeandikwa mwishoni mwa Injili ya Mathayo, na nitathibitisha baadaye kidogo kwamba aya za mwanzo na za mwisho za kila kitabu ni za kuongezwa baadaye. Aya zile siyo aya sahihi za Biblia.

3. Ya tatu katika aya 28:19 ya Mathayo neno mataifa limetumika kwa maana ya mataifa ya Israeli. Kama Biblia inavyosema kwamba: “Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote wa ulimwengu. (Luka 2:1). Kaisari Augusto alikuwa mtawala wa Roma tu. Hakuwa na mamlaka yoyote nje ya nchi yake juu ya ulimwengu. Katika aya hii amri iliyotolewa kwa ajili ya ulimwengu na ya nchi ya Roma tu iliyokuwa chini ya utawala wa Kaisari wala siyo ulimwengu wote. Hivyo ndivyo inavyoeleweka kauli ya Bwana Yesu aliposema: “Enendeni mkawafanye mataifa yote (ya Waisraeli) kuwa wanafunzi. (Mathayo 28:19).

## YESU ALILETA UPANGA

Sawa na mafundisho ya Biblia tumeelewa tayari kwamba Bwana Yesu alikuwa mtume kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Sasa tuone kwamba Bwana Yesu Kristo alileta kitu gani na alitumwa na nini?

Mwenyewe anatueleza lengo la kutumwa kwake, anasema:

1. Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani. La, sikuja kuleta amani, bali upanga. Kwa maana nalikuja kumfitinisha mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu. (Mathayo 10:34-35).
2. Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wa kike, naam na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. (Luka 14:26).
3. Je, mwadhani ya kwamba nimekuja kuleta amani duniani? Nawaambia la, sivyo, bali mafarakano. (Luka 12:51).
4. Bwana Yesu alitayarisha wafuasi wake kwa ajili ya kuleta fujo na vurugu na aliwaamrisha akawaambia: “Lakini sasa mwenye mfuko na auchukuwe, na mwenye mkoba vivyo hivyo, naye asiye na upanga akauze joho lake akanunuwe upanga. (Luka 22:36).
5. Siyo maneno tu bali katika maisha yake alionesha hata kwa vitendo vyake kwamba alikuwa mtu wa fujo. Biblia inasema kwamba: “Yesu aliingia ndani ya hekalu akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni. Akazipindua meza za wabadili fedha, na viti

vyao waliokuwa wakiuza njiwa." (Mathayo 21:12).
6. Akamwaga fedha za wenye kuvunja fedha, akizipindua meza zao. (Yohana 2:15).
7. Kwa sababu ya mafundisho yake, wanafunzi wake walikuwa wajeuri kiasi hiki kwamba walikuwa wakitumia upanga kwa ujasiri. Biblia inasema: "Na tazama, mmoja wao waliokuwa pamoja ya Yesu akanyoosha mkono wake, akaufuta upanga wake, akampiga mtumwa wa kuhani mkuu, akamkata sikio." (Mathayo 26:51).

Sasa mmesoma historia ya Bwana Yesu Kristo na mafundisho yake kuhusu kuleta fitina na fujo duniani na kuharibu amani ya watu. Na inashangaza wakati baadhi ya Mapadri wanatangaza au inaandikwa juu ya *'sticker'* za magari kwamba *"There is peace in the blood of Jesus"* yaani ipo amani katika damu ya Yesu. Ilhali yeye alikuwa siyo mwenye kuleta amani duniani bali upanga, fujo na fitina.

Sisi Waislamu tunaamini kwamba Bwana Yesu (Masihi) alikuwa Nabii wa Mwenyezi Mungu na alitumwa kwa lengo maalum, lililotajwa kwa ulimi wake katika Qur'an Tukufu kwamba: "Nisadikishaye yaliyo mbele yangu katika Taurati na kutoa habari njema ya Mtume atakayekuja nyuma yangu jina lake ni AHMAD." (QUR'AN 61:7).

Pia sawa na mafundisho ya Qur'an Tukufu, nabii Isa a.s. alifungamanishwa na amani katika maisha yake yote: "Na amani iko juu yangu, siku niliyozaliwa na siku nitakayokufa na siku nitakayofufuliwa kuwa hai." (19:34).

# LUGHA YA YESU

Kila mti hutambulika kwa matunda yake (Luka 6:44) na vile vile mtu anatambulika kwa ulimi na lugha yake kwamba anazo khulka za aina gani? Maana lugha ya mtu inaonesha masomo yake, tabia na khulka yake. Katika kitabu hiki tunampima Bwana Yesu Kristo sawa na maandiko ya Biblia.

Bila ya kupoteza muda wa wasomaji wangu, ningependa kuwaletea baadhi ya maneno na lugha ya Bwana Yesu aliyotumia katika uhai wake.

1. Wasioamini (wasio Waisraeli) wameitwa mbwa na nguruwe. (Mathayo 7:6).
2. Aliwaita watu wabaya: ”Enyi wazao wa nyoka” (Mathayo 12:34).
3. Mayahudi waliitwa: “Kizazi cha zinaa.” (Mathayo 12:40,, 16:4).
4. Mayahudi waliitwa “Wazinifu na wakosefu.” (Marko 8:38).
5. “Ole wenu waandishi na wafarisayo, wanafiki,” (Mathayo 23:16).
6. “Ole wenu viongozi vipofu.” (Mathayo 23:16).
7. “Enyi nyoka, wana wa majoka” (Mathayo 23:33).
8. “Watu wengine waliitwa mbwa.” (Mathayo 15:27).
9. Aliwaita manabii wenzake: “wote walionitangulia ni wevi na wanyang'anyi.” (Yohana 10:8).
10. Aliwaita wanafunzi wake: ”Enyi kizazi kisicho amini, kilichopotoka.” (Mathayo 17:17).
11. Akamwambia Petro “Nenda nyuma yangu Shetani.” (Mathayo 16:23).

12. Akamwambia mama yake: “Ewe mwanamke nina nini nawe? (Yohana 2:4).

13. Akasema mama yangu ni nani na ndugu zangu ni akina nani? (Mathayo 12:48).

14. Siku ya Kiyama atawaita wahubiri Wakristo: “Nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi mtendao maovu.” (Mathayo 7:23).

## WANAFUNZI WA YESU

Na majina ya hao mitume kumi na wawili ni haya; Wa kwanza Simon aliyeitwa Petro, na Andrea nduguye; Yakobo wa Zebadayo, na Yohana nduguye; Filipo, na Bartholomayo; Tomaso, na Mathayo mtoza ushuru; Yakobo wa Alfayo; na Thadayo; Simon Mkananayo, na Yuda Iskariote, naye ndiye mwenye kumsaliti. (Marko 10:2-4).

Kila mti hutambulika kwa matunda yake (Luka 6:44). Basi tuone mti uliopandwa na Bwana Yesu Kristo, matunda yake ni ya ladha gani? Madaraja yaliyofundishwa na Bwana Yesu tuone wanafunzi wake walikuwa wa aina gani? Yesu alipoleta imani, basi tuone kiwango cha imani ya waaminio wake.

Sina kawaida ya kuwafundisha watu kwa maneno yangu bali nawafundisha kulingana na maandiko yao matakatifu. Sasa tuone hali na imani ya wanafunzi wa Bwana Yesu.

1. Yesu alisema, hata sasa ninyi nanyi mngali hamna akili? (Mathayo15:16).

2. Alimwambia Petro kwamba; “Ewe mwenye imani haba, mbona uliona shaka? (Mathayo 14:31).

3. Petro alikanusha kuwa mfuasi wa Yesu mara tatu bali alimlaani. (Mathayo 26:69-75).

4. Yuda Iskariote alimuuza Yesu kwa shilingi 30 tu. (Mathayo 26:15).

5. Wakati Yesu alikuwa hatarini, wanafunzi waliendelea kulala). Mathayo 26:40-45; Marko 14:36:041).

6. Yuda alijinyonga. (Mathayo 27:5).

7. Imani ya wanafunzi: “Kwa sababu ya upungufu wa imani yenu” (Mathayo 17:20).

8. Ndipo wanafunzi wote wakamwacha wakakimbia. (Mathayo 26:50).

9. Wengi wataniambia siku ile; Bwana, Bwana hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri. Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu. (Mathayo 7:22-23).

Hapa juu mmesoma hali na imani ya wanafunzi wa Bwana Yesu sawa na Biblia. Lakini sisi Waislamu hatuamini kwamba Nabii yeyote anaweza kushindwa kiasi hiki kwamba asiweze kupata matunda ya juhudi yake na athari nzuri isitokee kwa mahubiri na mafundisho yake. Hata katika Qur'an Tukufu wanafunzi wa Bwana Yesu wametajwa kuwa mfano mzuri juu ya ulimi wa Bwana Yesu menyewe. Qur'an: “Enyi mlioamini! Muwe wasaidizi wangu kwa Mwenyezi Mungu kama alivyosema Isa bin Mariam kuwaambia wanafunzi (wake): Ni nani wasaidizi wangu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu? Wanafunzi wakasema: Sisi ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu.” (Qur'an 61:15).

## MIZANI YA IMANI YA WAKRISTO

Bwana Yesu Kristo alieleza mizani na alama za imani kama ifuatavyo:

1. Mkiwa na imani ya punje ya haridali, mtauambia mlima huu, ondoka hapa nenda kule, nao utaondoka; wala halitakuwapo neno lisilowezekana kwenu. (Mathayo17:20; 21:21; Marko 11:22-23, 9:23, Luka 17:6, 12, 13).
2. Bwana akasema: “Kama mngekua na imani kiasi cha chembe ya haridali mngeuambia mkuyu huu, ng'oka, ukapandwe baharini, nao ungewatii.” (Luka 17:7).
3. Yesu akajibu, akawaambia, Amin, nawaambia mkiwa na imani , msipokuwa na shaka, mtafanya si hilo la mtini tu, lakini hata mkiuambia mlima huu, ngo'ka ukatupwe baharini, litatendeka. na yoyote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea. (Mathayo 21:21-22)
4. Amin, Amin, nawaambieni, yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwani mimi naenda kwa Baba. (Yohana 14:12-13).
5. Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lolote nanyi mtatendewa. (Yohana 15:7).
6. Tena nawaambia, wawili wenu mtakapopatana duniani katika jambo lolote watakalo liomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. (Mathayo 7:3-12).

7. Ombeni nanyi mtapewa.... (Mathayo 7:3-12).

Katika mizani hii ya imani ya Wakristo, tumejua kwamba Mkristo atatambulika kwa alama zilizotajwa hapo juu. Tena hizi ni alama za imani ndogo sana ya chembe ya haridali. Lakini kama Mkristo atakuwa na imani kubwa ataweza kuonesha miujiza mikubwa zaidi.

Vilevile Mkristo mwenye imani ni yule ambaye ataweza kuonesha miujiza na hasa sawa na ya Bwana Yesu bali mikubwa zaidi kuliko yake. Sasa kwanza tutafute miujiza ya Bwana Yesu katika Biblia, tumeona baadhi yao kama ifuatavyo:

1. Kuponya wagonjwa (Mathayo 8:16, 9:22, na 15:21).
2. Kuponya walemavu (Mathayo 8:1-3).
3. Kuponya mabubu. (Mathayo 9:3-7; 12-22).
4. Kuponya mwenye kupooza upande mmoja (kiarusi) (Mathayo 8:5-13. 9:1-7, 12:22).
5. Kumponya mwenye kifafa. (Mathayo 17:14-19).
6. Kuponya mkono wenye ukoma. (Mathayo 12:15).
7. Kuponya mgongo uliopinda (Kibyongo) (Luka 13:10).
8. Kuwafufua wafu. (Mathayo 9:24).
9. Kugeuza maji kuwa pombe. (Yohana 2:1-9).
10. Chakula kidogo kitoshe watu elfu tano. (Mathayo 14:13-21).
11. Kutembea juu ya maji. (Mathayo 14:22-23).
12. Kuzuia tufani . ( Mathayo 8:23-33).

Hapa nimetoa baadhi ya mifano tu ya miujiza ya Bwana Yesu.

Kama Wakristo hawawezi kuonesha miujiza ya aina hii au alama ya imani yao sawa na Biblia, basi

mambo mawili yanathibitika.

A. Bwana Yesu pia hakuonesha mujiza wowote bali ni hadithi za kutungwa tu zisizo na ukweli ndani yake.

B. Siku hizi Mkristo yeyote hana imani sawa na chembe ya haridali, bali wote wameshapotea tayari na hawana alama au dalili yoyote ya imani.

Hali hizi zote mbili ni mbaya sana na za kutisha. Na dawa yake ni moja tu kwamba waingie katika dini ya Mwenyezi Mungu, ISLAM, baada ya kutambua umoja wa Mungu na Mtume Muhammad s.a.w. waila wataendelea kufedheheka siku hadi siku.

**TAMBIO:** Tunawapa Wakristo tambio (challenge) kwamba kama wanayo imani sawa na chembe ya haridali, watuoneshe miujiza iliyotajwa hapo juu. Mkristo mmoja au wawili au wajumuike wote, tunataka kuona miujiza tu ya imani yao, hata Pope au Kasisi wao ajitokeze.

## WAPINZANI WA YESU / ANTI CHRIST

Bwana Yesu Kristo alitumwa na Mwenyezi Mungu alifundisha mafundisho mazuri. Lakini baadaye wahalifu wake (Anti Christ) walikuja ambao waliharibu mafundisho yake mazuri. Leo ningependa kuwataja baadhi yao ambao wametenda kinyume cha vitendo na mafundisho yake. Kwa mfano:

**PAULO NI MPINZANI WA YESU**

Yesu alisema:

1. Katika njia ya Mataifa msiende. (Mathayo 10:5). Lakini Paulo akafundisha:

A. Nimekabidhiwa Injili ya wasiotahiriwa. (Wagalatia 2:7, maandishi ya Paulo).

B. Amewafungulia mataifa mlango wa imani. (Matendo ya Mitume 14:27).

2. Yesu alitahiriwa sku ya 8 (Luka 2:21). Yohana alitahiriwa siku ya 8 (Luka 1:59). Paulo alitahiriwa siku ya 8 (Wafilipi 3:5) Lakini yeye mwenyewe alipinga kutahiriwa (Wagalatia 5:2-6).

Yesu alisema:

3. Msidhani kuwa nalikuja kuitangua Torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya Torati haitaondoka, hata yote yatimie. Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atayezitenda na kuzifundisha , huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni. Maana nawaambia ya kwamba, Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni. (Mathayo 5:17-20).

Lakini Paulo anasema:

Sheria ni laana. (Wagalatia 2:16-21, 3:10-13). Warumi 7: yote).

4. Bwana Yesu alisema:

Msichukuwe dhahabu, wala fedha, wala mapesa mifukoni mwenu: (Mathayo 10:9).

Hivyo Wakristo wale ambao wanakusanya mali ni Madajjali (AntiChrist).

5. Bwana Yesu alisema: Lakini mimi nawaambia msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume mgeuzie na la pili. Na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia. (Mathayo 5:39-40). Hivyo Wakristo wale ambao wanagombana ni Madajjal (Ant Christ).

6. Yesu pia alikataza kuitwa Kristo: Ndipo alipowakataza wanafunzi wake wasimwambie mtu yeyote kwamba yeye ndiye Kristo. (Mathayo 16:20).

Hivyo Wakristo ambao wanatangaza kwamba Yesu ndiye Kristo ni Madajjal (Ant Christ).

7. Kwa maana nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu. (Mathayo 10:35, Luka 14:26, 12:51, 5:2)

Hivyo Wakristo ambao wanapenda amani wala hawatumii upanga ni Madajjal (Anti Christ).

## TABIRI ZA YESU

Kila mti hutambulika kwa matunda yake.” (Luka 6:44). Sawa na usemi huu wakati tunampima Bwana Yesu Kristo tunamkuta kwamba ameanguka vibaya sana. Ingawa sisi tumempenda na tumemuheshimu. Lakini kumpenda kwetu hakumsaidii. Maana Biblia inamuangusha vibaya sana. Kwa mfano:

(1) “Amini nawaambieni, pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapo muona mwana wa Adamu akija katika ufalme wake.” (Mathayo 16:28). Watu ambao walikuwa

pamoja naYesu na vizazi vyao zaidi ya hamsini wamekwisha kufa tayari. Hakuna mmoja wao ambaye ameweza kushuhudia, mwana wa Adamu (Yesu Kristo) akija katika ufalme wake.

Kwahiyo utabiri wa Yesu haujatimia bali imeonekana uwongo.

2. "Yesu akamwambia, amin, nawaambia ya kwamba ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya, atakapoketi Mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israel." (Mathayo 19:28).

Katika aya hii Bwana Yesu Kristo aliwabashiria wanafunzi wake kumi na wawili kuhusu mwisho mwema wa kiimani na kuwa viongozi wa makabila ya Waisraeli. Lakini mwanafunzi wake mmoja bwana Yuda hakumuasi tu bali alimuuza kwa shilingi thelathini. Kwa hivi alitoka katika imani na ufalme wa kiroho. Biblia inasema kwamba: "Wakati huo mmoja wa wale thenashara, jina leke Yuda Iskariote, aliwaendea wakuu wa makuhani, akisema, ni nini mtakacho nipa, nami nitamsaliti kwenu? Wakampimia vipande thelethini vya fedha." (Mathayo 26:14 -15).

3. Bwana Yesu Kristo alisema kwamba: "(Ewe Petro) nami nitakupa funguo za ufalme wa mbinguni, na lolote utakalo lifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni." (Mathayo 16:19). Katika aya hii Bwana Yesu alim'bashiria Petro kwamba ataendelea vizuri kiimani kwa hali ya juu, lakini hali inaonesha kwamba utabiri

huu wa Bwana Yesu ulivurugika vibaya mno. Hata inaonekana aibu kutaja utabiri ule. Biblia inasema kwamba: "Na Petro alikuwa ameketi nje behewani; kijakazi mmoja akamwendea, akasema, wewe nawe ulikuwapo pamoja na Yesu wa Galilaya. Akakana mbele ya wote, akisema, sijui usemalo. Naye alipotoka nje hata ukumbini, mwanamke mwingine alimuona, akawaambia watu walio kuwako huko, huyu alikuwa pamoja na Yesu Mnazareti. Akakana tena kwa kiapo, simjui mtu huyu. Punde kidogo, wale walio hudhuria wakamwendea, wakamwambia Petro, hakika wewe nawe u mmoja wao. Kwa sababu hata usemi wako wakutambulisha. Ndipo akaanza kulaani na kuapa na kusema, simjui mtu huyu." (Mathayo 26:69-74).

4. "Yesu akamwambia mwizi mmoja aliyekuwa pamoja naye msalabani: "Amin, nakuambia leo hii utakuwa pamoja nami peponi." (Luka 23:43). Aya hii inaonesha kwamba siku ya kusema habari hii Bwana Yesu Kristo na huyu mwizi wangeenda peponi kwa Baba lakini inaonekana kwamba utabiri huu haukutimia, maana baada ya siku ya tatu Yesu bado alikuwa duniani. Biblia inasema kwamba Yesu alimwambia, usinishike, kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu." (Yohana 20:17). Katika mifano hii ya Biblia tumejaribu kuonesha watu baadhi ya matunda ya tabiri za Yesu, na kila mmoja analalamika kwamba matunda haya ni machungu sana. Kwahiyo mti umetambulika kwa matunda yake.

**BWANA YESU HAKUFIA MSALABANI**

Msingi wa Ukristo siku hizi ni kifo cha msalaba cha bwana Yesu a.s. Mayahudi na Wakristo wanadhani kwamba Bwana Yesu alifariki juu ya msalaba, kifo cha laana.

A. Mayahudi walidhani hivi kwa sababu ya kupata nafasi ya kumkataa Bwana Yesu, kuwa wa kweli, maana Torati inasema kwamba "Aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu, (Kumbukumbu la Torati 21:23). Kwahiyo Mayahudi walitaka sana kumfisha Yesu msalabani ili athibitike kuwa mlaaniwa na mlaaniwa hawezi kuwa Nabii wa Mungu.

B. Wakristo walikubali kwamba Yesu alikufa msalabani kwa sababu waliambiwa kwamba Yesu amebeba dhambi za watu kwa kufa msalabani. Hivi wavivu wote ambao hawataki kufuata sheria ya Mungu, mara moja walikubali kwamba damu ya Yesu imetuokoa. (Wagalatia 3:13).

Qur'an Tukufu inapinga dhana hii na inatuelekeza kwenye ukweli wa jambo. Mwenyezi Mungu anasema kwamba: "Na kusema kwao: Hakika tumemuuwa Masihi Isa Mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu, Hali hawakumuuwa wala hawakumfisha msalabani, bali alifananishwa kwao (kama maiti). Na kwa hakika wale waliohitilafiana kwalo, Yakini wana shaka nalo, wao hawalijui hakika yake isipokuwa wanafuata dhana. Na kwa yakini wao hawakumuuwa. (Qur'an 4:158).

Baada ya kupata hakika ya hali katika Qur'an Tukufu, wakati tunasoma Biblia tunaona kwamba Biblia

pia inasadikisha kwamba Bwana Yesu hakufia msalabani. Nitaeleza hapa hoja za Biblia moja baada ya moja, zinazothibitisha kwamba Bwana Yesu hakufia msalabani kabisa.

1. Kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu. (Kumb. 21:23, Wagalatia 3:13). Basi mtu ambaye anafariki juu ya mti wa msalaba ndiye maluuni na maluuni anakuwa mbali na Mungu hawezi kuwa karibu na Mungu. Na mtu ambaye yu mbali na Mungu hawezi kuwa Nabii wa Mwenyezi Mungu.

Tunaamini kwamba sawa na Qur'ani na Biblia Bwana Yesu alikuwa Nabii wa Mungu, tena kachanguliwa na kubarikiwa. Kwahiyo haiwezikani kwamba Bwana Yesu afe kifo cha laana cha msalaba.

## UTABIRI WA KUSALIMIKA

2. Bwana Yesu mwenyewe katika uhai wake alitabiri kwamba atapata matatizo, lakini hatakufa kwa matatizo yale, bali atasalimika. Alieleza habari kwa mfano. Bwana Yesu akajibu, akawaambia, kizazi kibaya na cha zinaa chataka ishara, wala hakitapata ishara, ila ishara ya Nabii Yona. Kwani kama vile Yona alivyokaa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi. (Mathayo 12:39-40).

Aya hizi za Biblia zinaonesha kwamba Bwana Yesu hakuleta miujiza mingi bali wakati aliombwa kuonesha miujiza, aliwatayarisha watu na aliahidi kuwaonesha

muujiza mmoja tu.

Aliahidi kuonesha mujiza sawa na mujiza wa Nabii Yona. Mujiza wa Nabii Yona ni huu kwamba aliingia katika tumbo la nyangumi akiwa hai, alibaki ndani ya tumbo la nyangumi siku tatu akiwa hai, na wakati alipotoka tumboni mwa nyangumi alikuwa hai. Yaani kuingia katika tumbo la nyangumi na kukaa kwa siku tatu ndani na kutoka humo akiwa mzima, si kawaida bali mtu anakufa katika hali hii. Lakini Nabii Yona alijaaliwa kubaki hai katika muda huu wote kwa msaada wa Mwenyezi Mungu. Maana katika tukio hili la kukaa katika tumbo la nyangumi kwa siku tatu usiku na mchana siyo muujiza bali muujiza ni kuendelea na uzima na uhai katika hali ile ngumu. Hivyo ndivyo Bwana Yesu alitabiri kwamba atakuwa hai wakati akiingia na kukaa na kutoka katika tumbo ardhi / nchi.

Sasa tuchunguze kwamba Bwana Yesu aliwahi kutimiza ahadi yake au hapana. Ndugu Wakristo wanasema kwamba Bwana Yesu hakuweza kuonesha muujiza wake huu wa pekee. Kwa sababu wakati wa kuingia katika tumbo la radhi na muda wa kukaa humo alikufa. Kwahiyo hakuweza kutimiza ahadi yake. Na wakati hakuweza kuonesha muujiza wake wa pekee basi akaondoka bila muujiza wowote.

Lakini sisi Waislamu tunaamini kwamba Bwana Yesu Kristo alionesha mujiza ule aliowaahidi kuonesha. Maana aliingia katika tumbo la ardhi akiwa hai na alikaa huko siku tatu nzima. Sawa kabisa na hali ya Yona Nabii.

## 3. DAMU ILITOKA

Bwana Yesu Kristo alipigiliwa msalabani, damu yake ilimwagika na kwa sababu ya udhoofu na shida ile alizimia. Mayahudi waliokuwa na hamu sana kutangaza kifo chake cha laana, mara walitangaza kwamba Bwana Yesu ameshafariki msalabani ilihali alizimia tu. Biblia inasema kwamba: Lakini walipomjia Yesu na kuona ya kuwa amekwisha kufa hawakuvunja miguu. Lakini askari mmoja alimchoma ubavuni kwa mkuki, na mara ikatoka damu na maji. (Yohana 19:33-34).

Kifo cha Yesu juu ya msalaba ni dhana ya watu kwa sababu ya kuzimia kwake. Waila wakati alipochomwa mkuki ubavuni, mara ikatiririka damu na maji ambayo ni dalili ya uhai wake. Maana kutoka mfu au maiti damu haitoki kwa nguvu.

Bwana Yesu alikuwa bado msalabani na ilidhaniwa kwamba ameshafariki wakati ule, baada ya kuchomwa mkuki, kutoka kwa damu na maji, tena kwa nguvu ni dalili ya uhai wake. Kwahiyo tunaamini kwamba Bwana Yesu hakufia msalabani bali Mwenyezi Mungu alimsaidia kutimiza ahadi yake.

## 4. MAOMBI YALIKUBALIWA

Bwana Yesu Kristo wakati alikamatwa na Mayahudi na alikaribia kuteswa katika mikono ya watu, alimwomba Mungu sana. Alianguka mbele Yake,

alimkumbusha ahadi yake na alilia kuomba msaada wa Mwenyezi Mungu. Biblia inasema kwamba: Yesu alienda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi akaomba akisema; Baba yangu ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke walakini si kama nitakavyo mimi bali kama utakavyo wewe. (Mathayo 26:39).

Bwana Yesu Kristo alikuwa na yakini kwamba maombi yake yamekubaliwa na ndiyo maana alipoona hali imekuwa mbaya zaidi hata kinyume cha matarajio yake, akashangaa kwa kusema “Eloi, Eloi, Lama Sabakthani? Yaani Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniwacha? (Mathayo 27:46 na Marko 15:34).

Alilia hivyo kwa sababu Bwana Yesu alikuwa na yakini ya kukubaliwa maombi yake na ya kupata msaada wa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu Mwenyezi Mungu hukubali maombi ya waja wake, na Biblia inashuhudia kwamba maombi ya Bwana Yesu yalikubaliwa, inasema kwamba: “Yeye katika siku hizo za mwili wake alimtolea yule aliyeweza kumuokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na mchozi akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu. (Waebrania 5:7).

Mwenyezi Mungu mwenye uwezo wa kumuokoa na kuwasalimisha watu, alimwokoa Bwana Yesu pia kutoka kifo cha laana, kikombe cha mauti. Na baada ya kukubaliwa maombi Bwana Yesu alimshukuru sana Mungu wake, “akasema Baba nakushukuru kwa kuwa umenisikia nami nilijua ya kuwa wewe wanisikia siku zote. (Yohana 11:41-42).

Sasa wakati Biblia inatangaza kwamba Bwana Yesu

alimuomba Mungu kuondolewa kikombe na kifo cha msalaba, Mwenyezi Mungu alikubali maombi yake. Lakini leo wapo baadhi ya wapinzani wa Yesu ambao wanasema kwamba Mwenyezi Mungu hakujali maombi na machozi ya Yesu wala hakumsaidia kumsalimisha kutoka hila za Mayahudi. Na kikundi hiki cha Mapadri hata hawajali kufuta na kubadilisha aya za Biblia, ili waweze kutimiza matamanio na malengo yao. Hata wanasahau kwamba kwa njia hii wanamfedhehesha Bwana Yesu na wanamtenganisha na Mwenyezi Mungu.

Lakini sisi Waislamu tunaamini kwamba Bwana Yesu alikuwa mpendwa wa Mwenyezi Mungu na alikubaliwa maombi yake.

**5. <u>MPANGO WA HAKIMU</u>**

Bwana Yesu Kristo alikamatwa na kesi yake ilipelekwa katika mahakama ya Pilato. Hivyo hakimu, Bwana Pilato alichunguza na kugundua kwamba Bwana Yesu hana kosa lolote, bali anashitakiwa bure kwa sababu ya imani yake tu. Yeye alitaka kumwachia huru Yesu. (Mathayo 27:22, Luka23:20, Marko 15:9, Yohana 18:38-40 hadi 19:14-15 na Matendo 3:13). Vilevile mke wake aliogopeshwa ndotoni kuhusu Bwana Yesu. Kwahiyo alimshauri mumewe kumwacha huru Yesu. (Mathayo 27:19).

Lakini Mayahudi walikataa shauri la kumwacha huru Yesu. Basi bila shaka Bwana Pilato alitumia mbinu zingine kumsaidia Bwana Yesu kwa siri. Alipanga mpango wa aina hii kwamba maadui pia waridhike,

wasiwe na malalamiko, na Yesu naye asife juu ya msalaba. Kwahiyo alikuwa na yakini kwamba Yesu hawezi kufa juu ya msalaba. Hiyo ni sababu Pilato akastaajabu alipoambiwa kwamba Yesu amekwisha kufa. (Marko 15:44).

Bwana Pilato alijua kwamba mtu hawezi kufa katika muda wa saa chache wala wezi wawili pia hawakufariki juu ya misalaba yao waliopigiliwa pamoja na Yesu mpaka walipovunjwa miguu yao na wakauwawa. Wakati mtu wa kawaida hafi msalabani katika siku chache, itakuwaje Bwana Yesu afe mara moja, ambaye alikuwa na afya nzuri kiasi hiki kwamba aliweza kukaa na njaa kwa siku 40, usiku na mchana, bila kula chakula wala kunywa maji. (Mathayo 4:2).

## 6. YESU HAKUZIKWA KABURINI

Kawaida ni hii kwamba mtu anapofariki anazikwa kaburini. Lakini Bwana Yesu Kristo hakuzikwa kaburini bali alipumzishwa katika chumba fulani, ili atibiwe pale majeraha yake. Wakati walimuweka katika pango kisha watu wake walifunga mlango wa chumba kile kwa kuweka jiwe kubwa na wala sio kufukia kwa mchanga kama ilivyo kawaida ya kuzika. (Mathayo 27:60 na Marko 15:46).

Wenzake Bwana Yesu walijua vizuri kwamba Bwana Yesu hajafa. Kwa sababu hiyo hawakumzika, wakati Bwana Yesu alipumzika vya kutosha na alijisikia vizuri, alitoka kutoka chumba kile na alienda mahali pengine.

## 7. YESU ALIKUWA HAI

Wakati wa kuondoka kutoka chumba kile alituma ujumbe kwamba wanafunzi wake wamkute Galilaya. (Mathayo 38:7 na Marko 16:7). Baada ya kupata ujumbe huu wanafunzi wote walifika Galilaya. Baadhi yao walidhani kwamba Yesu ameshafariki tayari. Katika somo hili Biblia inasema kwamba: “Na walipokuwa katika kusema habari hiyo, yeye mwenyewe alisimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu. Wakashituka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona Roho. Akawaambia mbona mnafadhaika? Na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazama mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikeni-shikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo. Na baada ya kusema hayo aliwaonyesha mikono yake na miguu yake. Basi walipokuwa hawajaamini kwa majeraha, huku wakistaajabu, aliwaambia mna chakula chochote hapa? Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa. Akakitwaa, akala mbele yao. (Luka 24:36-43).

Tena Biblia inaondoa shaka ya kwamba Yesu hakufia msalabani bali aliendelea na uhai wake baadaye na aliendelea kukutana na wanafunzi wake. Biblia inasema: “Naye akiisha kusema hayo, akawaonyesha mikono yake na ubavu wake. Basi wale wanafunzi wakafurahi walipomwona Bwana. Basi Yesu akawaambia tena, Amani iwe kwenu; Kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi. (Yohana 20:20-21).

Bwana Tomaso bado alidhani kwamba huyu siyo Yesu bali ni Roho yake. Bwana Yesu aliondoa hata shaka yake pia. Biblia inasema kwamba: "Basi wanafunzi wengine wakamwambia, tumemuona Bwana. Akawaambia, nisipoziona mikononi mwake kovu za misumari, na kutia kidole changu katika mahali pa misumari, na kutia mkono wangu katika ubavu wake, mimi sisadiki hata kidogo. Basi, baada ya siku nne, wanafunzi wake walikutana ndani tena, na Tomaso pamoja nao. Akaja Yesu na milango imefungwa, akasimama katikati, akasema, Amani iwe kwenu. Kisha akamwambia Tomaso, lete hapa kidole chako; uitizame mikono yangu. Ulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu, wala usiwe asiye amini bali aaminiaye. (Yohana 20:26-27).

Kwa njia hizi zote Bwana Yesu alithibitisha kwamba tangazo lile la kifo na kuuawa kwake lilikuwa la uwongo. Yeye hakufia msalabani. Alisalimika na alihamia nchi nyingine za mashariki.

Sasa kabla ya kumaliza somo hili naomba wasomaji wasome andiko hili. Biblia inasema: " Basi, ikiwa Kristo anahubiriwa ya kwamba amefufuka katika wafu, mbona baadhi yenu husema kwamba hakuna kiyama ya wafu? Lakini kama hakuna kiyama ya wafu, Kristo naye hakufufuka; tena kama Kiristo hakufufuka, basi, kuhubiri kwetu ni bure na imani yenu ni bure. Naam, na sisi tumeonekana kuwa mashahidi wa uongo wa Mungu; kwa maana tulimshuhudia Mungu ya kuwa alimfufua Kristo, ambaye hakumfufua, ikiwa wafu

hawafufuliwi. Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka. Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu. Na hapo wao nao waliolala katika Kristo wamepotea. Kama katika maisha haya tumemtumaini Kristo, sisi tu maskini kuliko watu wote" (1Wakorintho 15:12-19).

Katika aya hizi imeelezwa kwamba kama watu hawatafufuka, Bwana Yesu pia hatafufuka. Na sote tunajua kwamba wafu watafufuka katika Akhera wala siyo katika dunia hii. Hivyo ndivyo Bwana Yesu pia atafufuka katika Akhera wala siyo katika dunia hii.
Biblia inasema kwamba: "Wafu hawawezi kurejea duniani." (Ayubu 7:9). Katika aya hizi jambo la pili limetajwa kwamba kama Kristo hakufufuka na wallahi hakufufuka, basi imani yenu ni bure. Mngalimo katika dhambi zenu. Yaani hakuna faida yoyote kuamini kifo cha laana na kufufuka kwake.

Habari ya tatu imeelezwa kwamba waliolala katika Kristo wamepotea. Na ya nne, hao ni maskini kuliko watu wote.

Enyi ndugu Wakristo, sisi tunawapendeni msife mioyo. Hamna kosa bali hamkujua. Basi sasa jiungeni na dini ya Kiislam. Karibuni sana, Dini ya Kiislam itawapatieni kila heshima. Na hiyo ni njia moja ya kusalimika, Muda wa kutosha mmeupoteza tayari. Sasa harakisheni kueleka kwenye njia iliyonyooka, Dini ya Mwenyezi Mungu yaani ISLAM. Karibuni sana.
Bwana Yesu hakufia msalabani wala hakufufuka duniani.

## 8. SAFARI YA KUTAFUTA KONDOO WALIOPOTEA

Bwana Yesu hakuweza kuuawa mapema bila kumaliza jukumu lake alilopewa na Mwenyezi Mungu. Mwenyewe anasema: “Na kondoo wengine ninao ambao si wa zizi hili, na hao nao imenipasa kuwaleta na sauti yangu wataisikia kisha kutakuwapo kundi moja na mchungaji mmoja. (Yohana 10:16).

Historia inatuonyesha kwamba makabila kumi ya Waisraeli walikimbilia mashariki kwa kutafuta amani na mawasiliano yalikatika baina yao. Kwa sababu hii wanawaita kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.

Bwana Yesu hakuweza kuyatafuta makabila haya kabla ya tukio la msalaba. Kwahiyo ilikuwa ni lazima asife mpaka atimize ahadi yake ya kuwatafuta kondoo waliopotea. Na kwa kweli Bwana Yesu alipitia nchi kadhaa wa kadha mwishowe alifika India, na aliwatafuta na kuwakuta kondoo hawa. Na kondoo walimtambua mchungaji wao, alipofariki alikuwa na wafuasi wengi wenye imani safi na imara wala hakufa kifo cha laana na cha kushindwa.

Baada ya miaka kadhaa wakati Mwenyezi Mungu alipomtuma Mtume Muhammad s.a.w. Hawa kondoo wote walimpokea Muhammad s.a.w. Sawa na mafundisho ya Bwana Yesu. Hiyo ni sababu katika nchi za Mashariki kondoo wanapatikana kwa uchache sana.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali soma kitabu Yesu Katika India cha Sayyidna Ahmad a.s. na Yesu Kafia Wapi? cha Maulana J.D. Shams. Vyote hivyo vinapatikana kutoka kwetu.

## KAFARA YA YESU HAISAIDII CHOCHOTE

Wakristo wanaamini ya kwamba Adamu na Hawa walifanya dhambi kisha wazao wao wote wanarithi dhambi hiyo (dhambi ya asili). Na Mwenyezi Mungu hawezi kuondoa adhabu ya dhambi ile bila kumwaga damu, na hakuna mtu yeyote anayeweza kuokoka bila ya kafara. Na anatolewa kafara ambaye hana dhambi yoyote. Na wakati wanadamu wote wanarithi dhambi hiyo, yeyote hawezi kutolewa kafara. Kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu alimtoa Bwana Yesu Kristo atolewe sadaka na damu yake iwe kafara ya dhambi za watu wote. Lengo la kutumwa kwa Yesu lilikuwa ni kuwaokoa wanadamu kwa kafara ya damu yake.

Katika kurasa zifuatazo nitachunguza na kuzipima hoja zote za Wakristo kuhusu kafara. Na itathibitika ya kwamba kafara ya Bwana Yesu haisaidii chochote.

(i) Mwenyezi Mungu ambaye ni Muumba wa ulimwengu aliye mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu hataki kafara ya watu kama alivyosema. “Nataka rehema wala siyo sadaka.” (Mathayo 12:7). Hiyo ni sababu wakati Nabii Musa alipotaka kujitoa kafara, Mwenyezi Mungu hakukubali mawazo yake. Biblia inasema ya kuwa: “Asubuhi yake Musa akawaambia watu, mmetenda dhambi kuu. Sasa nitakwenda juu kwa Bwana, labda nitafanya upatanisho kwa ajili ya dhambi yenu. Musa akarejea kwa Bwana akasema: “Aa!! watu hawa wametenda dhambi kuu, wamejifanyia mungu wa dhahabu. Walakini sasa, ikiwa utawasamehe dhambi yao na kama sivyo unifute,

nakusihi, katika kitabu chako ulichokiandika. Bwana akamwambia Musa, mtu yeyote aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta katika kitabu changu." (Kutoka 32:30-33).

(ii) Ikiwa lengo lilikuwa ni kuwasamehe watu, basi watu walisamehewa kwa maombi ya Nabii Musa tu. Wala haikuhitajika kumwagika damu ya mtu. Kama Nabii Musa mwenyewe alivyosema: "Nikaanguka nchi mbele za Bwana siku arobaini usiku na mchana, kama pale kwanza; sikula chakula wala kunywa maji ; kwa sababu ya makosa yenu yote mliyokosa, kwa kufanya yaliyo maovu machoni pa Bwana, kwa kumkasirisha. Kwa kuwa niliogopa hasira na makamio aliyowakasirikia Bwana kutaka kuwaangamiza. Lakini Bwana alinisikiza wakati huo nao. Bwana akamkasirikia sana Haruni akataka kumwangamiza; nikamwombea Harun naye wakati huo. (Kumbukumbu la Torati 9:18-20).

Siyo hiyo tu, bali wapo watu kadhaa wale ambao hawana dhambi bila ya kumwagwa damu ya Yesu. Kwa mfano, katika Biblia imesemwa kuwa: "Melkizedeki hana baba, hana mama, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu huyo adumu kuhani milele." (Waebrania 7:3).

Melkizedeki aliumbwa bila ya wazazi wawili, na huyo hana dhambi aliyorithi toka kwa wazazi. Vile vile Enoko alienda pamoja na Mungu. (Mwanzo 5:22). Enoko akiwa pamoja na Mungu kwa kuwa hakuwa na dhambi, kwa maana mwenye dhambi hawezi kumkaribia Mungu. Vile vile Biblia imesema kwamba Zakaria na mkewe Elizabeti hawakuwa na dhambi.

"Zamani za Herode, mfalme wa Uyahudi, palikuwa na kuhani mmoja jina lake Zakaria wa Zamu ya Abiya, na mkewe alikuwa mmoja wa uzao wa Haruni, jina lake Elizabeti na wote wawili walikuwa wenye haki mbele za Mungu wakiendelea katika amri zote za Bwana na maagizo yake bila lawama." (Luka 1:5-6).

Kama hawa wazee wawili hawakuwa na dhambi ndivyo vivyo mtoto wao Yohana hakuwa na dhambi. Imesemwa kuwa: "Sababu atakuwa mkuu mbele za Bwana hatakunywa divai wala kileo naye atajazwa roho mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye." (Luka 1:15). Sasa basi, ikiwa watu wote hawa walikuwa wema na hawakuwa na dhambi yoyote, kabla ya damu ya Yesu, sifa hizo walizipata vipi?.

(iii) Bibla inapinga na kufutilia mbali mawazo ya kuwa mtu anaweza kubeba dhambi za mtu mwingine. Kama Mwenyezi Mungu alivyosema:

(A) "Mababa wasiuawe kwa ajili ya watoto wao, wala watoto wasiuawe kwa ajili ya baba zao. Kila mtu auawe kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe." (Kumb. 24:16).

(B) Lakini kila mtu aipime kazi yake mwenyewe, ndipo atakapokuwa na sababu ya kujisifu ndani ya nafsi yake tu, wala si ya mwenzake." (Wagalatia 6:4). Wakati mtu hawezi kubeba dhambi za mtu mwingine, Mapadri wa leo wanahubiri kinyume na fundisho hili la Biblia kwa msingi gani?

(iv) Bwana Yesu hakujua lengo la kutumwa kwake kwamba ni kutolewa sadaka au kafara, kwa sababu hiyo alikuwa na hofu ya hali ya juu ya kuuwawa kwake. Ndiyo maana alijificha kama isemavyo Biblia: (A) "Basi

tangu siku ile walifanya shauri ya kumuwa kwahiyo Yesu hakutembea tena kwa wazi mpaka mji uitwao Eframu akakaa huko pamoja na wanafunzi wake." (Yohana 11:53-54).

(B) Maadamu mnayo nuru iaminini nuru hiyo ili mpate kuwa wana wa nuru. Hayo aliyasema Yesu, akaenda zake, akajificha wasimwone." (Yohana 12:36). Sasa mtu ambaye anasemekana kwamba alikuja kumwaga damu yake kwa ajili ya kuwaokoa watu kwa nini alijificha ficha? Na wakati alipotakiwa kumwaga damu alipiga mayowe? Kama tuirejeapo Biblia: "Na kama saa tisa Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema "Eloi, Eloi lamasabaktani? Yaani Mungu wangu! Mungu wangu mbona umeniacha? (Mathayo 27:46). Kama Yesu hakutaka kumwaga damu yake kwa hiyari yake, basi hii si sadaka wala kafara, bali ni kumshinikiza. Vilevile kama mtu anamsaidia masikini kwa hiyari yake, hii inakuwa ni sadaka, na kama ataporwa na masikini hiyo haitaitwa sadaka, bali hii itaitwa ni wizi au ujambazi.

## MTUME MUHAMMAD S.A.W. KATIKA BIBLIA

Tunasoma katika vitabu vya Mwenyezi Mungu kwamba Mtume ambaye anakuwa karibu kutumwa katika siku zijazo alama zake zinatajwa mapema ili watu waweze kujiandaa kumpokea. Kwa msingi huu wakati tunasoma Biblia tunakuta kwamba Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. ametajwa kwa alama na ishara zilizo wazi, Baadhi ya mifano nitaeleza katika kurasa zijazo.

**(1) <u>MTUME MFANO WA MUSA</u>**

Nabii Musa alitubashiria kwamba Mwenyezi Mungu alisema: "Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, Nami nitatia maneno yangu kinywani mwake naye atawaambia yote nitakayo mwambia. Hata itakua mtu asiye sikiliza maneno yangu atakayoyasema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake. Lakini nabii atayenena neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumuagiza kulinena, au atakaye nena katika jina la miungu wengine, nabii yule atakufa," (Kumbu. 18:18-20).

Katika aya hizi alama zifuatazo zimetajwa:

(1) Atakaye tumwa atakuwa nabii wa Mwenyezi Mungu.

(2) Atatokea miongoni mwa ndugu za Waisraeli yaani atakuwa mwana wa Ismail.

(3) Atakuwa mfano wa Musa.

(4) Atapewa maneno na amri za Mungu, yaani sheria.

(5) Atasema kwa jina la Mwenyezi Mungu.

Sisi Waislamu tunaamini kwamba katika aya zilizotajwa juu Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. ametabiriwa lakini ndugu Wakristo wanadhani kwamba Bwana Yesu Kristo ametabiriwa katika aya hizi. Kuhakikisha habari hii, sasa nitaeleza sifa moja baada ya nyingine.

(1) Aliyetabiriwa atakuwa nabii wa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo sisi Waislamu tunaamini kwamba Muhammad s.a.w. ni nabii wa Mwenyezi Mungu. Lakini ndugu Wakristo wanaamini kwamba Yesu ni mwana

wa Mungu bali Mungu mwenyewe. Kwa hiyo Bwana Yesu ameikosa sifa ya kwanza na Muhammad s.a.w. ameipata.

(2) Mtume aliyetabiriwa katika aya hizi atatokana miongoni mwa ndugu wa Waisraeli na ndugu za Waisraeli ni wana wa Ismail. Bwana Yesu Kristo hakutokea kutoka ndugu wa Israeli bali mwenyewe alikuwa mwana wa Israeli. Lakini Muhammad s.a.w. ametokea katika ukoo wa Ismail ambao ni ndugu za Waisraeli. Kwahiyo sifa ya pili pia Bwana Yesu ameikosa na Muhammad s.a.w. ameipata.

(3) Mtume aliyetabiriwa katika Taurat atakuwa mfanao wa Musa, sasa tuone kati ya Muhammad s.a.w. naYesu ni nani anayefanana na Musa.

(a) Musa alizaliwa na wazazi wawili na Muhammad s.a.w. pia alizaliwa na wazazi wawili, lakini Yesu alizaliwa na mzazi mmoja. Kwahiyo Muhammad s.a.w. anafanana na Musa lakini Yesu hafanani naye.

(b) Musa aliajiriwa na wengine kwa ajili ya kuchunga wanyama wao, vilevile Muhammad s.a.w. aliajiriwa na wengine kuchunga wanyama wao na kuwasaidia katika biashara yao. Lakini Yesu hakuajiriwa kwa aina yoyote. Kwahiyo Muhammad s.a.w. amefanana na Musa. Na Yesu ameikosa sifa hiyo pia.

(c) Nabii Musa a.s. alioa na vilevile Mtume Muhammad s.a.w. alioa. Lakini sawa na dhana ya Kikristo Yesu hakuoa. Kwahiyo Muhammad s.a.w. anafanana na Musa na Yesu hafanani naye. Sifa hiyo pia Yesu ameikosa.

(d) Musa alipewa kitabu cha sheria, Taurati chenye

amri kumi na vilevile Muhammad s.a.w. alipewa kitabu cha sheria Qur'an. Lakini Yesu hakupewa kitabu chochote cha sheria. Kwahiyo Muhammad s.a.w. amefanana na Musa na Yesu hafanani na Musa. Sifa hiyo pia ameikosa.

(e) Musa alihamia nchi nyingine kwa sababu ya upinzani mkali. Muhammad s.a.w. naye pia alihamia nchi nyingine kwa sababu ya upinzani mkali toka kwa makafiri. Lakini sawa na imani ya Kikristo Yesu hakupata nafasi ya kuhamia nchi nyingine kutokana na upinzani alioupata kutoka kwa Mayahudi. Kwahiyo Muhammad s.a.w. anafanana na Musa. Yesu hafanani naye, sifa hii pia ameikosa.

(f) Musa alipigana na maadui zake na aliwashinda. Muhammad s.a.w. pia alipigana na aliwashinda maadui zake. Lakini Yesu hakupigana na maadui zake na wala hakuwashinda. Hivyo Muhammad s.a.w. amefanana na Musa, lakini Yesu hafanani na Musa hata kidogo.

(g) Nabii Musa a.s. alipata nafasi ya kuwatawala wapinzani wake, vilevile Mtume Muhammad s.a.w. pia alipata nafasi ya kuwatawala wapinzani wake . Lakini Yesu hakupata kuwatawala wapinzani wake. Kwahiyo Yesu hafanani na Musa, Sifa hii pia ameikosa.

(h) Musa alipata wanafunzi wengi, vilevile Muhammad s.a.w. alipata malaki ya wafuasi. Lakini Yesu katika maisha yake alipata wanafunzi thenashara tu (kumi na wawili) tena wenye imani haba (hafifu). Kwahiyo Muhammad s.a.w. anafanana na Musa a.s. Bwana Yesu sifa hii pia ameikosa.

(i) Wakati Nabii Musa alipofariki, alifariki kabisa. Vilevile Mtume Muhammad s.a.w. alipofariki, alifariki kabisa. Lakini sawa na dhana ya Wakristo wakati Bwana Yesu alipofariki, alifariki kwa siku tatu tu. Kwahiyo kutokana na sifa hii pia Muhammad s.a.w. anafanana na Musa a.s. na Bwana Yesu hafanani naye hata kidogo.

Sasa mmeona kwamba Muhammad s.a.w. anafanana na Musa mia kwa mia. Kuanzia kuzaliwa kwake hatua kwa hatua mpaka kifo chake. Lakini Bwana Yesu Kristo hafanani na Musa hata safari moja.

4. Katika utabiri wa awali imetajwa kwamba nabii yule atapewa maneno na amri za Mwenyezi Mungu, yaani sheria ya Mungu, na kwa kweli Muhammad s.a.w. alipewa amri za sheria yaani Qur'an Tukufu. Lakini Bwana Yesu Kristo hakupewa chochote kama anavyosema mwenyewe: “Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua Torati au Manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza.” (Mathayo 5:17). Kwahiyo Muhammad s.a.w. amepata sifa hii na Bwana Yesu ameikosa.

(5) Nabii yule atasema kwa jina la Mwenyezi Mungu. Wakati tunasoma sheria iliyoletwa na Muhammad s.a.w. tunakuta ya kwamba kila sura iliyo kwenye Qur'an Tukufu inaanza kwa jila la Mwenyezi Mungu. Vilevile Mtume Muhammad s.a.w. alitufundisha dua ya kufanya kila kazi ianze kwa jina la Mwenyezi Mungu. Lakini Bwana Yesu Kristo katika maisha yake hakusema kwa jina la Mwenyezi Mungu wala hakuwafundisha wafuasi wake kuomba kwa jina la Mwenyezi Mungu. Kwahiyo Muhammad s.a.w. amepata

sifa hii na Bwana Yesu ameikosa.

Alama zote zilizotajwa katika Torati 18:18-20 zinapatikana katika dhati ya Muhammad sa.w. Lakini BwanaYesu Kristo hapati hata moja kati ya hizo. Lengo letu siyo kumpinga Bwana Yesu bali kumtaja ambaye kweli kweli ametabiriwa. Waila tunamuamini Bwana Yesu na tunamheshimu sawa sawa kabisa.

Katika aya 18:19 ya Kumbukumbu la Torati imetajwa kwamba "Mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake." Kwa hiyo tunawakaribisha ndugu Wakristo wampokee Nabii yule ili wasalimike kuadhibiwa na Mwenyezi Mungu. Tunawashauri hivi kwa kuwa tunawapenda na vilevile ni amri ya Mwenyezi Mungu kumkumbusha asiyejua.

## BISHARA YA PILI

"Akasema Bwana alitoka Sinai akawaondokea kutoka Seir, aliangaza katika kilima cha Parani, akaja na elfu kumi za watakatifu upande wa mkono wake wa kuume palikuwa sheria ya motomoto. (Kumb. 33:2). Katika aya hii milima mitatu imetajwa kuhusu mitume watatu, Nabii Musa aliyetokea toka mlima Sinai, Nabii Isa aliyetokea toka mlima Seir, na Nabii wa tatu alitokea kutoka kilima cha Parani baada ya Isa, ambaye si yeyote isipokuwa Mtume Muhammad s.a.w. ambaye alama yake imetajwa kwamba akaja na elfu kumi za watakatifu. Sasa bila shaka ni Mtume Muhammad s.a.w. ambaye ametokea kutoa katika milima ya Parani. Maana "Ismail alikaa katika jangwa la Parani

na mama yake" (Mwanzo 21:21). Na ni Muhammad s.a.w. tu ambaye aliingia siku ya ushindi wa Makka pamoja na masahaba wake watakatifu elfu kumi. Hiyo ndiyo sababu Mapadri waliozoea kubadilisha Biblia katika kila chapa, wakalibadilisha pia tamko hili la watakatifu elfu kumi ili bishara hii isieleweke. Katika Biblia ya lugha ya Kiswahili badala ya watakatifu elfu kumi wameandika MARBATH - KADESH, ilhali Marbath Kadesh siyo neno la Kiswahili wala hawajui lina maana gani. Isipokuwa kufanya hivyo ni kumwaga takataka juu ya neno la Mwenyezi Mungu.

Tena alama ya yule Nabii imetajwa kwamba atakuja na sheria motomoto, yaani sheria mpya kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Basi Mtume Mtukufu Muhammad s.a.s. amekuja na kitabu kipya cha sheria motomoto, yaani Qur'an Tukufu.

## BISHARA YA TATU

"Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamuwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja, huyo roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayo yasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake." (Yohana 16:12-13).

Katika andiko hili Bwana Yesu Kristo anaeleza kwamba uwezo wa kipaji cha watu wa wakati wake ulikuwa mdogo hawangeweza kustahimili mafundisho yote ya sheria. Kwahiyo alitabiri kwamba mwingine

atakuja baadaye ambaye ametajwa kama roho wa kweli. Yeye ataleta mafundisho kamili ya sheria kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Huyu ni Mtume Muhammad s.a.w. ambaye ameitwa katika Qur'an Roho itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Vilevile ni yeye ambaye ameleta sheria kamili yaani Qur'an Tukufu kutoka kwa Mwenyezi Mungu baada ya Bwana Yesu Kristo. Kwahiyo hakuna shaka kwamba Roho wa kweli aliyetajwa katika aya hii ni Mtume Muhammad s.a.w.

## BISHARA YA NNE

Bishara hii yenye nguvu imo katika Mathayo 21:33-40. Hii ni mojawapo ya methali za Yesu ambamo ndani yake mna utabiri wa kufika Mtume Mtukufu. Bishara yenyewe ni hii:- "Kulikuwa na mtu mwenye nyumba naye alipanda shamba la mizabibu, akalizungushia ua, akachimba shimo la shinikizo ndani yake, akajenga mnara akapangisha wakulima akasafiri. Wakati wa matunda ulipokuwa karibu akawatuma watumishi wake kwa wale wakulima, wapokee matunda yake. Wale wakulima wakawakamata watumishi wake, huyu wakampiga na huyu wakamwua, na huyu wakampiga kwa mawe. Akawatuma tena watumishi wengi kuliko wa kwanza, ikawa tena vile vile. Mwisho akamtuma mwanawe kwao, akisema watamsitahi mwanangu.

" Lakini wale wakulima walipomwona yule mwana, wakasemezana wao kwa wao, Huyu ni mrithi haya na tumwue, tuutwae urithi wake, Wakamkamata

wakamtupa nje ya shamba la mizabibu, wakamwua. Basi atakapokuja yule bwana wa shamba la mizabibu atawatendaje wale wakulima? Wakamwambia, Atawaangamiza vibaya wale wabaya, na shamba la mizabibu atawapangisha wakulima wengine, watakaomlipa matunda kwa wakati wake. Yesu akawaambia, Hamkupata kusoma katika maandiko, Jiwe walilolikataa waashi, hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni. Kwa sababu hiyo nawambia, Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa lingine lenye kuzaa matunda yake. naye aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika, na yeyote ambaye litamwangukia litamsaga tikitiki. Wakuu wa makuhani na Mafarisayo waliposikia mifano yake, walitambua ya kuwa anawanenea wao. Nao walipotafuta kumkamata, waliwaogopa makutano, kwa maana wao walimwona kuwa nabii,"

Katika methali hii iliyo nzuri Yesu ameeleza historia ya mfululizo wa kuja kwa Mitume. Ni wazi hapa kwamba shamba la mizabibu ndiyo ulimwengu, wakulima maana yake ni walimwengu kwa jumla, matukio ambayo bwana wa shamba alitaka kuvuna ndiyo wema, uaminifu na ucha-Mungu, watumishi ndiyo manabii wa Mungu waliokuja duniani mmoja baada ya mwingine; mwana ndiye Yesu aliyekuja baada ya mfululizo wa manabii wengi. Mwana huyu aliadhibiwa na wakulima. Baada ya kusema mambo haya, Yesu ameendelea kunena juu ya "Jiwe" walilolikataa waashi, hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni." Jiwe lililokataliwa ndiyo wazao wa Ismaili, waliodharauliwa na wana wa Isihaka.

Kulingana na bishara hii ya Yesu, mtu mmoja angekuwa jiwe kuu la pembeni - “Muhuri wa Manabii,” katika lugha mashuhuri ya Qur'an tukufu - hangekuwa nabii wa cheo cha chini, bali mfano wa manabii atakayeleta Sheria ya mwisho na kamili toka kwa Mwenyezi Mungu. Kuinuliwa kwa Nabii toka katika nyumba ya Ismaili lilionekana jambo geni, kwani wengi katika mfululizo wa manabii wa hapo mbele walitoka katika nyumba ya Isihaka (Israel). Lakini Yesu anasisitiza ya kuwa Mwenyezi Mungu ataondoa ufalme wake kutoka nyumba ya Israeli na kuwapa wana wa Ismaili, watakaotoa matunda yake; yaani wana wa Ismaili ndiyo watakaokuwa taifa litakalodumisha ucha-Mungu na ibada ya Mwenyezi Mungu duniani. Kila mtu anaweza kuona hapa ya kuwa hapana mtu yeyote aliyedai utume baada ya Yesu, na akafanikiwa, isipokuwa Mtume mtukufu Muhammad s.a.w. Ni yeye ambaye mafundisho yake yalihitilafiana na dini ya Mayahudi na akavunja kabisa nguvu za dini hiyo. Ni yeye ambaye taifa lake lilidharauliwa na kuchukiwa. Kama tulivyosema hapo mbele, nabii Muhammad s.a.w. ndiye mjumbe wa Mungu wa pekee aliyejaaliwa kushinda maadui zake wote katika uhai wake, hivyo ni yeye tu ambaye ndiye lile jiwe ambalo yeyote aliyeanguka juu yake alivunjika-vunjika na yeyote liliyemwangukia likamsaga tikitiki. Wakristo wamekosea sana kwa kudhani Yesu ndiye “Jiwe” linalotajwa hapa. Lakini wanasahau ya kuwa Yesu alikuwa Mwisraeli, hali yeye amesema “Ufalme wa Mungu utaondolewa kutoka kwa Waisraeli na kupewa

taifa jingine,"  yaani Waismaili. Isitoshe, ikiwa jiwe ni Yesu, basi ingefaa kufahamishwa aliwasaga akina nani tikitiki?

## BISHARA YA TANO

"Kwa sababu hiyo  nawaambia, ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa lingine lenye kuzaa matunda yake.: (Mathayo 21:43). Katika aya hii Bwana Yesu Kristo  amewajulisa wanafunzi wake na Waisrael kwamba  ufalme wa Mungu utaondolewa kwao na litapewa taifa lingine. Taifa  lingine lilotajwa hapa ni taifa la wana wa Ismaili lililo kataliwa na kubughudhiwa na  wa Israil.

## BISHARA YA SITA

"Kwa maana nawaambia hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, amebarikiwa ajae kwa jina la Bwana," (Mathayo 23:39). Katika aya hii Bwana Yesu Kristo mwenyewe amesema kwamba yeye anaondoka hataonekana tena lakini amebashiri kuja kwa M'barikiwa mwingine na ambaye atakuja kwa  jina la Bwana Mungu. Na baada ya  kifo cha bwana Yesu Kristo  ametumwa Mtume Muhammad s.a.w. tu kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambaye  ameleta sheria, kila sura  yake inaanza  kwa jila la Bwana Mungu. Vilevile ametufundisha dua za nyakati za vitendo mbalimbali. Kila dua inaanza kwa jina la Bwana Mungu.

## MWANA MKUU WA IBRAHIM

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. alitumwa na Mwenyezi Mungu kuwa rehema kwa Ulimwengu. Wakristo kwa sababu ya kushindwa kumpokea, sasa wanaendelea kumchafua huyo Mtume wa amani na wa shani. Hasa wanajaribu kukosoa ukoo wake. Katika upinzani huu wanasahau kwamba wanamdhalilisha hata Nabii Ibrahim a.s. ambaye ni mheshimiwa na mkubwa wao pia.

Katika kurasa zijazo nitajaribu kujibu shutuma za Mapadri kulingana na maandishi ya Biblia.
Na itathibitika vizuri kwamba ukoo wa Muhammad s.a.w. ni safi na wenye baraka.

## IBRAHIM MUME WA HAJIRA

Wakristo kwa husuda zao hawapo tayari kukubali kwamba Bi Hajira alikuwa mke wa Nabii Ibrahim, na lengo lao linakuwa kumtoa Nabii Ismaili kuwa mwana wa Ibrahim. Hata hawajali wala hawatafakari kwamba kama Bi Hajira si mke wa Nabii Ibrahim a.s., kulikuwa na uhusiano gani baina yao. Ibrahim, Nabii wa Mungu alitenda nini, kwa matokeo yake Ismail alizaliwa? Biblia inasema wazi kwamba Bi Hajira alikuwa mke wa Nabii Ibrahim. Imeandikwa kwamba: “Sara, mkewe Ibrahim akamtoa Hajira Mmisri mjakazi wake baada ya kukaa katika nchi ya Kanaan miaka kumi, akampa Abraham mumewe awe mkewe.” (Mwanzao 16:3).

**ISMAILI MWANA ALIYEAHIDIWA, MWENYE BARAKA**

Siyo hayo tu kwamba Bi Hajira alikuwa mke wa Nabii Ibrahim a.s. bali Hajira alishukiwa na Malaika ambaye alimuahidi mwana wa kiume. Biblia inasema kwamba:- "Malaika wa Bwana akamwambia: Hakika nitauzidisha uzao wako, wala hautahesabika jinsi utakavyo kuwa mwingi. Malaika wa Bwana akamwambia: Tazama wewe una mimba utazaa mwana wa kiume nawe utamwita jina lake Ishmaeli maana Bwana amesikia kilio cha mateso yako." (Mwanzo 16:10-11).

Tena Biblia inasema kwamba: "Na kwa habari za Ismail nimekusikia, Nimem'bariki, nitamzidisha nami nitamwongeza sana sana. Atazaa maseyidi kumi na wawili nami nitamfanya awe taifa kuu." (Mwanzo 17:20).

**ISMAILI MWANA WA IBRAHIM A.S.**

Biblia inasema wazi wazi kwamba, Ismaili alikuwa mwana wa Ibrahim: "Yule mwana wa Hajira Mmisri, ambaye alimzalia Ibrahim, anafanya dhihaka." (Mwanzo 21:9). Vilevile Biblia inasema kwamba Ibrahim akamtwaa Ismaili mwanawe." (Mwanzo 17:23). Sasa bila shaka yoyote inaonekana hasa kwamba Ismaili alikuwa mwana wa Ibrahim. Kama ni kosa ni la Ibrahim wala siyo la Ismail. Kwa sababu Ismail alizaliwa baada ya Ibrahim kukutana na Hajira kimwili.

**MWANA MKUU WA IBRAHIM A.S.**

Sisi Waislamu tunaamini kwamba Ibrahim alimuoa Bi Hajira kama mke mdogo na Mwenyezi Mungu

alimsaidia mke mdogo atangulie kumzalia Ibrahim mumewe mwana wa kiume. Bi Hajira anazo haki zote, kwa mumewe vilevile Ismail anazo haki zote kwa babaye Ibrahim. Ismail siyo mwana tu wa Ibrahim bali ni mwana mkuu wa Ibrahim. Biblia inasema kwamba: “Naye Ibrahim alikuwa mtu wa miaka themanini na sita, hapo Hajira alipomzalia Ibrahim Ismail.” (Mwanzo 16:16).

Baada ya kupita miaka mingi wakati Ismail alipokuwa kijana mkubwa Bi Sara alipata mimba na Isihaka alizaliwa. Biblia inasema kwamba: “Naye Ibrahim alikuwa mtu wa miaka mia alipozaliwa mwana wake Isaka.” (Mwanzo 21:5). Kwa maandiko haya imejulikana kwamba Ismail ndiye aliyekuwa mwana mkuu wa Ibrahim, Isihaka alikuwa mdogo wa miaka kumi na nne kuliko Ismaili.

**MUNGU ALIMSIKIA ISMAIL A.S.**

Wakati inajulikana kwamba Bi Hajira alikuwa mke halali wa Ibrahim na Ismail ndiye mwana mkuu wa Ibrahimu, tunawashauri ndugu Wakristo waache husuda yao ya kurithi katika imani kuhusu Ismail ambaye ni babu wa Muhammad s.a.w. Maana Hajira alikuwa akishukiwa na Malaika, na Mungu alimsikia na alim'bariki Isamail. Biblia inasema kwamba: “ Mungu akasikia sauti ya kijana, Malaika wa Mungu akamwita Hajira kutoka mbinguni, akamwambia una nini Hajira? Usiogope maana Mungu amesikia sauti ya kijana huko aliko. Ondoka ukamwinue kijana, ukamshike mkononi mwako, kwa kuwa nitamfanya taifa kubwa.” (Mwanzo 21:17-18).

## MUNGU YU PAMOJA NA ISMAIL

Sasa nafasi gani imebaki ya kubaguliwa kwa Ismail baada ya kusoma maandiko haya yote matakatifu? Na kwa ajili ya kusisitiza jambo hili ningependa kuwaongezeeni hapa chini andiko moja tu. Andiko ambalo linathibitisha kwamba Mungu alikuwa pamoja na Ismaili. Biblia inasema kwamba: "Mungu akawa pamoja na huyu kijana naye akakua akakaa katika jangwa la Parani mama yake akamtwalia mke katika nchi ya Misri." (Mwanzo 21:20-21).

Ndugu Wakristo mmeona kwamba Mungu yupo pamoja na Ismaili sasa ninyi mnataka kuwa upande gani? Upande wa Mungu ambaye ni pamoja na Ismail au upande wa mwingine? Karibuni katika Islam, ili muweze kushuhudia baraka zile zilizoahidiwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kizazi cha Ismail.

## UJAJI WA YESU MARA YA PILI

Katika Qur'an tukufu na Hadithi imetabiriwa kwamba Bwana Yesu Kristo atarudi mara ya pili. Katika Islam tumeelewa kwamba Bwana Yesu alikufa kifo cha kawaida na mfu hawezi kurudi duniani tena. Kwahiyo ujaji wake utakuwa wa kiroho siyo kwamba aje mwenyewe.

(1) Biblia pia inatuambia kwamba ujaji wa mara ya pili na ushukaji kutoka mbinguni hautimii kwa kidhahiri bali unatimia kwa kiroho kwa sura ya mtu mwingine, kama (2 Wafalme 2:11) inaeleza kwamba Eliya nabii

alipaa mbinguni na Malaki 4:5 inatabiri kwamba Eliya nabii atarudi. Lakini Mayahudi mpaka leo wanamsubiri Eliya nabii kutoka mbnguni. Lakini hajashuka wala hawezi kuja.

Wakati Bwana Yesu Kristo aliulizwa kuhusu ujaji na ushukaji wa Eliya nabii, alijibu kwamba Eliya amekwisha fika tayari na alimuashiria Yohana M'batizaji. (Mathayo 11:14, Yohana 17:17).

Hivyo sawa na jibu la Bwana Yesu Kristo Eliya nabii alizaliwa hapa hapa duniani kwa sura mpya na kwa jina jipya. Hivyo ndivyo Bwana Yesu Kristo atakuja mara ya pili kwa namna ya mfano, kwa sura mpya na jina jipya. Bali amekwisha fika tayari kwa jina la Ahmad a.s. ambaye ni Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.

## 2. SI YESU BALI NI MWINGINE

Bwana Yesu amesema kwamba: “Kwa maana nawaambia, hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana.” (Mathayo 23:39). Katika aya hii Bwana Yesu Kristo mwenyewe amesema kwamba yeye hataonekana kamwe. Kwa sababu baada ya kifo, mtu haonekani dunani. Na kama utabiri useme kuhusu ujaji wake mara ya pili, basi utabiri ule unatimia kwa ujaji wa mtu mwingine ambaye anakuja kwa sifa, tabia hata kwa jina la marehemu. Hivyo ndivyo Bwana Yesu Kristo amesema kwamba yeye mwenyewe hataonekana bali mwingine atakuja kwa jina la Bwana Yesu Kristo.

Katika istilahi ya Biblia Yesu pia anaitwa Bwana (Matendo 1:24, Warumi 4:24, 2 Wakorintho 4:5, 13:14, 11:31; Wagalatia 1:3, 6:14, 6:18 na 1:17; Waefeso 1:15-17, 6:23-24; Petro 1:2,8-16).

Basi sawa na utabiri Bwana Yesu Kristo ameshafika tayari mara ya pili kwa sura ya Sayyidna Ahmad a.s., mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Mwenye masikio na asikie. Sasa mwenye kuja ameshafika tayari, hakuna faida ya kumsubiri ambaye amefariki zamani. Maana wafu hawarudi tena duniani. (Ayubu 7:9-10). Kwa hiyo karibuni sana kumpokea ambaye ametumwa na Mwenyezi Mungu kwa sifa, khulka na tabia ya Bwana Yesu Kristo.

## 3. ATAKUJA WAKATI WATU WASIOUTEGEMEA

Biblia inasema kwamba: "Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari, kwa kuwa katika saa msiyodhani mwana wa Adamu yuaja. " (Mathayo 24:44). Yaani kuja kwa Bwana Yesu mara ya pili itakuwa kwa ghafla kulingana na dhana ya watu. Watu wataendelea kumsubiri na itajulikana kwamba kumbe yeye ameshafika tayari. Na hivyo ndivyo ilivyotokea tayari. Wakristo wanamsubiri wakiwa na mategemeo na dhana tofauti. Ilhali Bwana Yesu ameshafika tayari na mamilioni ya watu wameshampokea. Lakini Wakristo bado wanalala katika dhana yao. Kwahiyo tunawaamsha ndugu Wakristo kwamba mwenye kuja ameshafika. Karibuni ili mpate kuokoka.

**4. YESU ATAKUJA KAMA MWIZI**

Bwana Yesu Kristo alisema kwamba: “Basi kumbuka jinsi ulivyopokea, na jinsi ulivyo sikia. Yashike hayo na utubu walakini usipo kesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayo kuja kwako.” (Ufunuo wa Yohana 3:3). Vilevile Matahayo 24:43. Na Petro 3:10 inaeleza kwamba Bwana Yesu Kristo atakuja kama mwizi. Aya hizi hazina maana ya kwamba Yesu ni mwizi bali imetajwa hali ya mwizi. Kama mwizi anavyokuja bila mategemeo ya watu, vilevile Bwana Yesu Kristo atakuja bila mategemeo ya watu.

Kama watu wanafunga milango kuhofia kwamba mwizi ataingia kupitia katika mlango, lakini yeye anaingia katika dirisha. Mlinzi anakaa mlangoni kulinda nyumba lakini mwizi anaruka ukuta mwingine na ana ingia ndani. Hivyo ndivyo Bwana Yesu Kristo atakavyo kuja mara ya pili. Na kweli imetokea kwamba watu walitegemea ashuke kutoka mbinguni lakini yeye ametokea katika kijiji cha Qadiani. Watu walidhani kwamba atakuwa yuleyule mwana wa Israeli. Lakini amekuja kutoka katika ukoo wa Farsy, watu walitegemea kwamba atakuja kubeba msalaba lakini aliyekuja amekuja kuvunja msalaba. Yaani Sayyidna Ahmad a.s. mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.

**5. ATAKUJA KAMA UMEME**

Biblia inasema kwamba: ” Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyo kuwa kuja kwake

Mwana wa Adamu." (Mathayo 24:27).

Katika aya hii imetajwa kwamba katika ujaji wake wa mara ya pili, Bwana Yesu atatokea kutoka nchi ya Mashariki na ujio wake utatambulikana na utakubaliwa katika nchi za magharibi pia kwa haraka. Na tunamshukuru Mungu hivyo ndivyo imetokea kwamba Masihi Aliyeahidiwa ametokea katika nchi ya India iliyoko mashariki ya dunia na ujumbe wake umepokelewa sana katika nchi za magharibi. Na kweli tunaweza kusema kwamba amekuja kama umeme utokao mashariki kuelekea magharibi.

## 6. KUPATWA KWA JUA NA MWEZI

Biblia inasema kwamba: "Lakini mara baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka mbinguni na nguvu za mbinguni zitatikisika. Ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapo omboleza, nao watamuona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingine." (Mathayo 24:29-30). Bishara hii inapatikana katika Qur'an na Hadithi pia . Wakati Sayidina Ahmad a.s. alidai kwamba yeye ni Masihi Aliyeahidiwa, kisha mashahidi hawa wawili walitokea. Mwezi ulipatwa tarehe 21 Machi, 1894 (13 ya Ramadhani) na jua lilipatwa tarehe 6 Aprili, 1894 (28 Ramadhani) baada ya kuona ishara hizi Sayydina Ahmad a.s. alikuwa mtu pekee duniani aliye tangaza kwamba jua na mwezi vimepatwa kuonesha ukweli wake.

## 7. VITA, TAUNI NA NJAA VITATOKEA

Biblia inasema kwamba: "Kisha aliwaambia taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme. Kutakuwa na matetemeko makubwa ya nchi, na njaa na tauni mahali mahali, na mambo ya kutisha na ishara kuu kutoka mbinguni." (Luka 21:10-11). Katika aya hizi alama zilizotajwa za kuja kwa Bwana Yesu mara ya pili ni zifuatazo vita baina ya taifa na taifa, ufalme na ufalme, matetemeko ya ardhi na njaa na tauni. Alama hizi zote zimetimia tayari wakati wa mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya bali tangu wakati ule Mwenyezi Mungu anaendelea kurudia rudia ishara hizi.

## 8. GHARIKA NA MAFURIKO YA MAJI

Biblia inasema kwamba: "Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyo kuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya gharika watu walivyo kuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambuwe hata gharika ikaja ikawachukuwa wote, ndivyo kutakavyo kuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." (Mathayo 24:37-39). Katika aya hizi imetajwa kwamba wakati wa ujaji wa mara ya pili wa Bwana Yesu Kristo gharika na mafuriko ya maji vitakuja kama siku ya Nuhu. Na hivyo ndivyo tunaona na tunasoma katika magazeti kila nchi na kila bara mafuriko na gharika kila mwaka yanatokea makubwa kiasi hiki kwamba magari na magari moshi yanazama, miji na vijiji vinaangamizwa

na maji hata watu wale ambao hawakushuhudia gharika na mafuriko katika nchi yao pia siku hizi wanaathirika na hayo.

Ndugu Wakristo alama zote za ujaji wa Bwana Yesu Kristo zimetimia na yeye amekwisha fika tayari. Kwahiyo msichelewe bali mpokeeni ambaye mnamsubiri tangu zamani na hiyo ni njia yenu ya kuokoka.

## KUPINGANA KWA MAANDIKO YA BIBLIA

Mtu yeyote hapendi kwamba katika mazungumzo yake hitilafu ipatikane. Wala hapendi kusikia kwamba maneno yake yanapingana. Ikiwa mtu hapendi hivi, itakuwaje kwamba maneno ya Mungu yapingane. Maandiko yanayopingana hayawezi kuwa ya kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hii Mwenyezi Mungu amesema kwamba: “Je! hawaitafakari Qur'ani? Na kama ingalitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, bila shaka wangalikuta ndani yake hitilafu nyingi.” (Qur'an 4:83). Hapa chini nitaeleza baadhi ya mifano inayothibitisha kupingana vibaya sana kwa maandiko ya Biblia.

### (1) MTU AU WANYAMA:

Biblia inasema kwamba: “Mungu alimfanya mnyama wa mwitu kwa jinsi yake na mnyama wa kufugwa jinsi yake, na kila kitu kitambaacho juu ya nchi kwa jinsi yake. Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Mungu akasema na tumfanye mtu kwa mfano wetu,

kwa sura yetu, wakatawale wale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama wa nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akamuumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimuumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba." (Mwanzo 1:25-27).

Aya hizi zinapatikana katika ukurasa wa kwanza kabisa wa Biblia zinazosema kwamba Mwenyezi Mungu aliwaumba wanyama na ndege na kila chenye kutambaa juu ya nchi. Kisha alimuumba mtu. Kwa bahati mbaya ukurasa wa pili wa Biblia unapingana na maandiko ya ukurasa wa kwanza. Biblia inasema kwamba: "Bwana Mungu akasema, si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamleta Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu ikawa ndilo jina lake." (Mwanzo 2:18-19).

Aya hizi zinasema waziwazi kwamba mtu alitangulia kuumbwa, wanyama na ndege wakaumbwa baadaye. Je, neno la Mungu linaweza kupingana kiasi hicho?

**(2) TORATI SI KITABU CHA MUSA**

Tunaposoma kichwa cha Torati kinasomeka hivi:- "Kitabu cha tano cha Musa, kiitwacho Kumbukumbu la Torati, haya ndiyo maneno - Musa aliyowaambia Israeli wote ng'ambo ya Yordan barani" (Kumbukumbu la Torati 1:1). Mwanzo wa kitabu hiki tumesoma kwamba Torati ni kitabu cha Musa alionena

mwenyewe. Na wakati tunafika mwisho wa kitabu hiki tunasoma hivi: “Basi Musa mtumishi wa Bwana akafa huko Moab, kwa neno la Bwana akamzika bondeni katika nchi ya Moab, kukabili Beth Peor, Lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo.” (Kumbukumbu la Torati 34:5-6).

Aya hizi zinaonesha kwamba Torati iliandikwa baada ya kifo cha Musa. Hiyo ni sababu kwamba mwandishi wake ameeleza kifo na kaburi la Musa. Tena inaonekana kwamba Taurati iliandikwa miaka mingi kupita baada ya kifo cha Musa; maana mwandishi anaandika kwamba mpake leo hakuna mtu anayejua kaburi la Musa.

### 3. <u>MWIZI MMOJA AU WAWILI</u>

Biblia inasema kwamba: “Pia wale wanyang'anyi waliosulubiwa pamoja naye walimshutumu vilevile.” (Mathayo 27:44). Aya hizi za Biblia zinasema kwamba wezi wote wawili walimtukana Yesu. Na ajabu ni hii kwamba, tusomapo Luka, yeye anasema hivi: “ Na mmoja wa wale wahalifu waliotungikwa alimtukana, akisema, je! wewe si Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi. Lakini yule wa pili akamjibu akamkemea, akisema, wewe humuogopi hata mungu, nawe u katika hukumu hiyo hiyo.” (Luka 23:39-40).

Katika aya hizi kinyume cha aya za kwanza inaonekana kwamba mwizi mmoja alimtukana Yesu wala siyo wote wawili. Juu ya jambo hili Mabwana Mathayo na Marko wamesimama upande mmoja na Bwana Luka anawapinga.

## 4. JE, YUDA ALIJINYONGA?

Biblia inasema kwamba: “(Yuda) akavitupa vipande vya fedha katika hekalu, akaondoka, akaenda akajinyonga.” (Mathayo 27:5). Aya hii inasema kwamba mwanafunzi Yuda aliyemuuza Yesu kwa vipande thelathini vya fedha, alijinyonga. Lakini tunaposoma katika kitabu cha Matendo ya Mitume, Bwana Paulo anasema hivi: “Basi mtu huyu alinunua konde kwa ijara ya udhalimu, akaanguka kwa kasi akapasuka, matumbo yake yote yakatoka.” (Matendo ya Mitume 1:18). Katika aya hii imeonekana kwamba Yuda hakujinyonga bali alianguka na akapasuka na hivi maandiko ya Biblia yanapingana.

## 5. FEDHA ZILITUMIKA WAPI?

Biblia inasema kwamba: “(Yuda) akavitupa vile vipande vya fedha katika hekalu, akaondoka, akaenda, akajinyonga.” (Mathayo 27:5). Katika aya hii inatajwa kwamba Bwana Yuda alivitupa vipande thelathini vya fedha katika Hekalu, lakini kitabu kingine cha Biblia kinasema kinyume chake. Imeandikwa kwamba: “Basi mtu huyu alinunua konde kwa ijara ya udhalimu, akaanguka kwa kasi akapasuka, matumbo yake yote yakatoka.” (Matendo 1:18).

Wasomaji wapendwa; mmesoma kwamba mwandishi mmoja wa Biblia anatuhadithia tukio maalum kinyume kabisa na mwenzake.

## 6. MATHAYO SIYO MATHAYO

Biblia inasema kwamba: “Naye Yesu alipokuwa akipita kutoka huko aliona mtu ameketi forodhani aitwaye Mathayo, akamwambia nifuate, akaondoka, akamfuata,” (Mathayo 9:9). Katika aya hii inaonekana waziwazi kwamba Bwana Mathayo siyo mwandishi wa Injili bali ni mtu mwingine ambaye anahadithia kisa cha kitabu kisemacho “Injili kama ilivyoandikwa na Mathayo Mtakatifu.”

## 7. MWANA NI MKUBWA KULIKO BABA

Biblia inasema kwamba:

(A) “Yohoramu alikuwa na umri wa miaka thelathini na miwili alipoanza kutawala, akatawala miaka minane huko Yerusalemu.” (2 Mambo ya Nyakati 21:5).

(B) “Alikuwa na umri wa miaka thelathini na miwili alipoanza kutawala akatawala huko Yerusalemu miaka minane, akafariki, bila kutamaniwa, wakamzika mjini mwa Daudi, ila si katika makaburi ya wafalme.” (2 Mambao ya Nyakati 21:20).

Katika aya hizi mbili imeandikwa kwamba Bwana Yehoramu mfalme wa Yerusalemu alipofariki alikuwa na umri wa miaka arobaini, mara baada ya kifo chake aliyeshikilia mahala pake pa kutawala ni mwanawe mdogo, sasa tuone Biblia inasemaje kuhusu umri wa mwana mdogo wakati wa kushikilia utawala. Imeandikwa kwamba: “Nao wenyeji wa Yerusalemu walimfanya Ahazia mwanawe mdogo awe mfalme mahala pake. Maana wakubwa wote wamekwisha kuuawa na kikosi cha watu waliokuja matuoni pamoja

na Waarabu. Hivyo akatawala Ahazia mwana wa Yehoramu mfalme wa Yuda. Ahazia alikuwa na umri wa miaka arobaini na miwili alipoanza kutawala. Akatawala mwaka mmoja huko Yerusalemu na jina la mamaye aliitwa Athalia binti Omri." (2 Mambo ya Nyakati 22:1-2).

Ndugu wasomaji mmesoma katika aya za kwanza wakati mfalme Yehoramu alipofariki alikuwa na umri wa miaka arobaini. Mara baada ya kifo chake mwanawe mdogo Ahazia akashikilia mahali pake pa kutawala, akiwa na umri wa miaka arobaini na miwili. Hivi inaonekana kwamba Ahazia mwana wa Yehoramu alizaliwa miaka miwili kabla ya baba yake mzazi. Sasa akili gani itakubali falsafa hii na hisabati ya Biblia kwamba mtoto azaliwe kabla ya baba mzazi, na hii ni dalili ya kutosha kwamba, Biblia siyo neno la Mungu wala haifai siku hizi bali imepitwa na wakati.

## 8. <u>YESU ALITANGUA TORATI AU HAPANA</u>

Bwana Yesu Kristo alisema kwamba "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua Torati na manabii, la, sikuja kutangua bali kutimiliza kwa maana amin nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi wala nukta moja ya Torati haitaondoka hata yote yatimie. "Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo na kuwafundisha watu ataitwa mdogo kabisa katika ufame wa mbinguni." (Mathayo 5:17-19).

Tukiendelea kusoma mbele, haipiti hata dakika moja tunaona kwamba Bwana Yesu tayari amekwisha sahau aliyoyasema, na anaanza kusema kinyume

kabisa na amri za Torati. Anasema kwamba: “Mmesikia kwamba imenenwa jicho kwa jicho, na jino kwa jino, lakini mimi nawaambieni msishindane na mtu muovu; lakini akupigaye shavu la kuume mgeuzie la pili, mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia.” (Mathayo 5:38-40).

Sasa Bwana Yesu Kristo ambaye alikuja kuitimiza Torati wala si kuitangua, mara anaonekana anaanza kuzipinga amri za Torati zinazopatikana katika “Kutoka 21:24’ Mambo ya Walawi 24:20, Kumbukumbu la Torati 29:21.” Na hivi inaonekana kwamba ilikuwa kuna hitilafu kubwa katika maneno ya Bwana Yesu. Na mtu anachanganyikiwa kabisa kwa mafundisho yake. Tayari tumetangulia kuthibitisha ya kuwa Bwana Paulo ndiye mhalifu wa Yesu, Bwana Yesu alikuja kuimarisha sheria ya Taurati, lakini Bwana Paulo anaibadilisha kama alivyosema kwamba: “Maana ukuhani ule ukibadilika hapana budi sheria nayo ibadilike.” (Waebrania 7:12).

## 9. <u>HARUNI ALIFIA WAPI?</u>

Biblia inasema kwamba “Haruni akakwea mlima wa Hori, kwa amri ya Bwana, akafa hapo katika mwaka wa arobaini baada ya Wana wa Israeli kutoka katika nchi ya Misri mwezi wa tano, siku ya kwanza ya mwezi.” (Hesabu 33:38). Kitabu kingine cha Musa kinapinga mahali pa kufia na imeandikwa kwamba “ (Wana wa Israeli wakasafiri kutoka visima vya Bene -Yaakani kwenda Mosera; Haruni akafa huko, akazikwa huko; na ELeazari mwanawe alitumika utumishi wa ukuhani badala yake.” (Kumbukumbu la Torati 10:6).

Sasa hiyo ni moja wapo ya hitilafu kuhusu sehemu aliyofia Haruni.

## 10. <u>WATOTO WA BENJAMINI NI WANGAPI?</u>

Biblia inasema kwamba “Wana wa Benjamin, Bela na Bakeri na Yedaiali, watatu.” (1Mambo ya Nyakati 7:6). Aya hii inaonesha watoto wa Benjamin ni watatu tu, lakini tusomapo mlango ufuatao unasema: “Naye Benjamin akamzaa Belo mzaliwa wake wa kwanza na wa pili Ashbeli na watatu Ahiramu; na wa nne Noha na wa tano Rafa. (1Mambo ya Nyakati 8:1-2).

Aya ya kwanza inasema watoto wa Benjamin ni watatu, ambapo andiko la pili linasema kuwa Benjamin alikuwa na watoto watano. Hivyo hii nayo ni hitilafu mojawapo kubwa katika maandiko ya Biblia.

Ndugu wasomaj mmeshuhudia jinsi maandiko ya Biblia yanavyopingana. Hapo tumekutajieni mifano kumi tu kuwaonesheni uharibifu wa Kitabu hicho; waila Biblia nzima imejaa mambo ya ovyo ovyo na iliyochezewa na mikono ya waandishi kama isemavyo yenyewe: “Mwasemaje, sisi tuna akili na Torati ya Bwana tunayo pamoja. Lakini tazama kalamu yenye uwongo ya waandishi imeifanya kuwa uwongo.” (Yeremia 8:8).

Kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu ameleta sheria mpya tena motomoto ambayo ni Qur'ani. Kwahiyo ninawakaribisha ndugu Wakristo kwenye maandiko ya sheria ya kisasa inayoongoza katika mambo yote.

## MAONGEZEKO KATIKA BIBLIA

Katika somo lililopita tumejifunza kwamba Biblia imeshapitia katika mikono ya waandishi wake. Sasa tunawaleteeni baadhi ya mifano michache inayojielezea kuwa ni ya kuongezeka katika Biblia kuwa si neno la Mungu wala siyo maneno ya manabii. Kwa mfano katika kitabu cha Musa kiitwacho Kumbukumbu la Torati kinaanza hivi: “Haya ndiyo maneno ya Musa aliyowaambia Israeli wote ng'ambo ya Yodani barani, katika Araba lililoelekea Sufu, kati ya Parani, na Tofeli na Labani, na Hazerothi na Dizahabu. Ni mwendo wa siku kumi na moja kutoka Horebu kwa njia ya mlima Seiri mpaka Kadesh-barnea. Ikawa mwaka wa arobaini mwezi wa kumi na moja, siku ya kwanza ya mwezi. Musa akawaambia wana wa Israeli kama yote aliyopewa na Bwana ya kuwaamuru; alipokwisha kumpiga Sihoni mfalme wa Waamori, aliyekuwa akikaa Heshboni, na Ogu mfalme wa Bashani, aliyekuwa akikaa Ashtarothi iliyo katika Edrei; ni ng'ambo ya Yordan katika nchi ya Moabu, alipoanza Musa kufunua Torati hii, akisema...” (Kumbukumbu la Torati 1:1-5).

Katika aya hizi inaonekana waziwazi ya kwamba maneno haya si ya Mungu akiongea na Musa na wala si maneno ya Musa aliyoongea na Mungu, bali ni maneno ya mwandishi asiyejulikana kama utangulizi. Maneno ya Musa yanaanzia msitari wa sita. Na hivyo aya hizo tano za mwanzo zimeongezwa katika kitabu cha Musa.

## 2. MAITI ANAONGEA?

Biblia inasema kwamba: “Basi Musa mtumishi wa Bwana akafa huko katika nchi ya Maoabu kwa neno la Bwana. Akamzika bondeni katika nchi ya Moabu kukabili Beth Peuri. Lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo hii. Musa alikuwa wa miaka mia na ishirini alipokufa jicho lake halikupofuka wala nguvu za mwili wake hazikupunguka. Wana wa Israeli wakamwombolezea Musa katika uwanda wa Moabu siku thelethini. Basi siku za maombolezo ya matanga ya Musa zikaisha. Na Yoshua mwana wa Nuni alikuwa amejaa roho ya hekima, maana Musa alikuwa amemwekea mikono yake juu yake. Wana wa Israeli wakamsikiliza, wakafanya kama Bwana alivyomwamuru Musa. Wala haijawahi tena katika Israeli Nabii kama Musa ambaye Mungu alimjua uso kwa uso katika ishara zote za marejeo yote ambayo Bwana alimtuma kuyatenda katika nchi ya Misri kwa Farao na kwa watumishi wake wote na kwa nchi yake yote.” (Kumbukumbu la Torati 34:5-12).

Aya hizi ni za kitabu cha Musa. Wakati Musa alipofariki alizikwa hata watu wake wakasahau kaburi lake. Na kitabu chake bado kinaendelea kuandika. Na Mungu alimpatia aya hizi nane ilhali yeye tayari alikwisha zikwa. Au maiti ya Musa iliendelea kuhubiri maneno haya katika kaburi lake. Na mambo yote haya hayawezikani. Isipokuwa tukubali kwamba baada ya kifo cha Musa, mwandishi fulani aliongeza maneno haya katika kitabu cha Musa. Kwahiyo si sahihi kusadiki kuwa Biblia ni neno la Mungu, bali ni ngano (hadithi za

kubuniwa) za waandishi.

3. Kitabu cha Yoshua kinaanzia hivi: “Ikawa baada ya kufa kwake Musa mtumishi wa Bwana, Bwana akamwambia Yoshua, Mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa akasema” (Yoshua 1:1) . Maneno yote hayo si maneno ya Mungu kuongea na Yoshua, na wala si maneno ya Yoshua aliyoongea na Mungu, bali ni maneno ya mwandishi yeyote.

4. Aya ya kwanza katika kitabu cha Waamuzi inasomeka hivi: “Ikawa baada ya kufa Yoshua, wana wa Israeli wakamuliza Bwana wakisema, ni nani atakayekwea kwanza kwa ajili yetu juu ya Wakanani, ili kupigana nao?” (Waamuzi 1:1). Maneno ya aya hii yanaonesha kwamba siyo ya Mwenyezi Mungu wala ya Yuda ambaye wakati ule alikuwa bado hajatumwa bali ni maneno ya mwandishi yeyote aliyejaribu kuboresha kitabu cha Waamuzi.

5. Kitabu cha Mathayo kinaanza hivi: “Injili kama alivyoandika Mathayo Mtakatifu. Ambapo tunapofika Mathayo 9:9 msitari unasomeka hivi: “Naye Yesu alipokuwa akipita kutoka huko aliona mtu ameketi forodhani, aitwaye Mathayo akamwambia nifuate. Akaondoka na akamfuata.” Aya hii inaonesha kwamba maneno haya siyo ya Bwana Mathayo, bali mtu mwingine ameeleza habari za Mathayo, tena ni maneno yaliyoongezwa baadaye katika kitabu kinachosemwa kuandikwa na Mathayo.

6. Kitabu cha Mambo ya Walawi kinaanza hivi: “Kitabu cha tatu cha Musa kiitwacho Mambo ya Walawi. Na tunaposoma aya yake ya kwanza ya kitabu hiki

inasomeka hivi: "Bwana alimwita Musa, na kusema naye kutoka katika hema ya kukutania, akamwambia." Aya hii inaonesha kuwa siyo maneno ya Mungu kwa Musa wala siyo maneno ya Musa mwenyewe. Maana maneno ya Musa yanaanzia katika aya ya pili. Kwahiyo imethibitika kwamba ni maneno ya kuongezwa katika Biblia.

7. Kitabu cha Musa kiitwacho Mambo ya Walawi kinaishia hivi: "Haya ndiyo maagizo, Bwana aliyomwagiza Musa kwa ajili ya wana wa Israeli katika mlima wa Sinai." (Mambo ya Walawi 27:34). Aya inaonesha kwamba siyo neno la Mungu wala neno la Musa bali ni maneno ya mwandishi ambaye hatambuliki.

8. Kitabu cha nne cha Musa kiitwacho Hesabu kinaanzia hivi: "Bwana akanena na Musa katika bara la Sinai hemani mwa kukutania, siku ya kwanza ya mwezi wa pili katika mwaka wa pili baada ya kutoka kwao nchi ya Misri akamwambia." Maneno haya siyo ya Musa kwa sababu maneno yake yanaanza katika msitari wa pili. Kwahiyo aya ya kwanza ni ya kuongezwa katika kitabu cha Musa.

9. Aya ya mwisho ya kitabu cha Musa kiitwacho Hesabu inasomeka hivi: "Haya ndiyo maagizo na hukumu ambayo Bwana aliwaagiza wana wa Israeli. Kwa mkono wa Musa, hapo katika nchi tambarare za Moabu, karibu na Yordani, hapo Yerko." Sasa ni wazi kuwa maneno hayo siyo ya Musa bali ni ya mtu mwingine ambaye amejasiri kuongeza maneno yake katika kitabu cha Musa.

10. Kitabu cha kwanza cha Suleimani kiitwacho Mithali kinaanzia hivi: “Mithali ya Suleimani, mwana wa Daudi mfalme wa Israeli.” Ni wazi kwamba aya hii ni ya kuongezwa baadaye wala siyo ya Suleimani.

11. Wimbo ulio bora kinaanzia hivi: “Wimbo ulio bora wa Suleimani.” (1:1) Ni wazi kuwa aya hii siyo ya Suleimani, bali ni ya mtu mwingine iliyoongezwa.

12. Kitabu cha Nabii Isaya kinaanzia hivi: “Haya ni maneno ya Isaya mwana wa Amoizi aliyoyaona katika habari za Yuda na Yerusalemu, siku za Uzia na Yothamu na Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda.” (Isaya 1:1).

Maneno ya Isaya yanaanzia katika aya ya pili, maneno ya aya ya kwanza siyo ya Isaya bali ni ya mwandishi mwingine asiyejulikana aliyeongeza katika kitabu cha Isaya.

Ndugu wasomaji mmeshuhudia kwamba aya kadhaa zimeongezwa na waandishi katika Biblia na tumewatajieni baadhi ya mifano michache tu, waila Biblia imechafuliwa vibaya sana. Kwahiyo siku hizi hatuwezi kuitegemea, kama zamani maandiko ya Biblia yalikuwa matakatifu, basi siku hizi siyo matakatifu bali yamechafuliwa kabisa na heshima ya Biblia imeangushwa.

Kama mtu anakuwa na chakula kizuri na baadaye aone kwamba uchafu fulani umeangukia katika chakula hawezi kuridhika kukitumia chakula kile isipokuwa kipofu. Hivyo ndivyo ilivyo hali ya maandiko ya Biblia yameangukiwa na uchafu wa nje maana maneno ya watu ni uchafu tu mbele ya maneno ya Mungu na ya

manabii. Kwahiyo nawashauri wasomaji wenzangu wajihadhari na watazame vizuri kabla ya kufuata maandiko hayo.

(a) "Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu yeyote atayaongeza, Mungu atamwongeza hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki." (Ufunuo wa Yohana 22:18).

(b) "Msiliongeze neno niwaamurulo wala msilipunguze, mpaka kuzishika amri za Bwana, Mungu wenu, niwaamuruzo." (Kumbukumbu la Torati 4:2).

(c) Neno niwaagizalo lolote liangalieni kulifanya usiliongeze wala usilipunguze." (Kumbukumbu la Torati 12:32).

Viongozi wa Kikristo na wachapaji wa Biblia wanaongeza-ongeza maneno yao katika Biblia wameonywa tayari katika kitabu cha Mungu kama sisi tukifuata nyayo zao na tukifuata mafundisho yao lazima sisi pia tutaadhibiwa pamoja nao.

Kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu aliteremsha sheria mpya, Qur'an inayofaa kwa hali zote.

## AYA ZA BIBLIA ZILIZOFUTWA

Ndugu wasomaji mmesoma jinsi aya zilivyoongezwa katika Biblia na mifano yake kadhaa mmeiona. Sasa ningependa kuwaelezeni kwamba zipo aya kadhaa pia zilizofutwa katika Biblia kwa makusudi, kwa sababu haziungi mkono imani ya siku hizi ya Mapadri. Kwahiyo badala ya viongozi wa Kikristo kujirekebisha sawa na kitabu cha Mungu,

wanayabadilisha bali wanaharibu maandiko matakatifu kwa kufuata matamanio yao.

Biblia inawaongoza sana wale ambao wanaondoa aya za Mwenyezi Mungu. Biblia inasema kwamba: “Na mtu yeyote akiondoa lolote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamuondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.” (Ufunuo wa Yohana 22:19).

Aya za Biblia zilizofutwa katika chapa mpya*

Mathayo: (12:47; 17:21; 18:11; 21:44; 23:14).

Zilizofutwa nusu ya pili. (6:13; 27:49).

Marko: ( 7:16; 9:44-46; 11:26; 15:49).

Luka: (17:36; 22:43-44; 23:17; 24:12; 24:40).

Yohana: (5:4 na 5:3 nusu ya pili).

*Chapa mpya ya:

1. Revised Standard Version.
2. The Good News Bible.
3. The Holy Bible.
4. The Bible James Version.
5. Biblia Habari Njema.

## BIBLIA INAVYOWADHALILISHA WANAWAKE

Sheria nzuri ni ile ambayo inatimiza mahitaji ya watu wote. Vilevile inawaheshimu barabara bila kuwabagua kwa njia yoyote. Akina mama ni sehemu ya lazima na muhimu katika dunia. Tunaposoma Biblia, tunaona

kuwa inawabagua wanawake bali inawafedhehesha vibaya sana kiasi hiki kwamba hata hawapewi haki za msingi za binadamu. Nitaeleza hapa baadhi ya mifano tu:

**1. Wasisuke nywele wala wasivae nguo za thamani**

Biblia inasema kwamba: "Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele; wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani." (1 Timotheo 2:9).

**2. Mwanamke asifundishe wala asitawale**

Sawa na Biblia mwanamke hana uhuru wowote. Hawezi kuwafundisha wengine wala hana ruhusa ya kumtawala mwanamume. Biblia inasema kwamba: "Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu." (1 Timotheo 2:12).

**3. Wanawake wasihubiri**

Biblia inawanyanyasa wanawake kiasi hiki kwamba wamenyimwa haki ya kuongea kanisani. Wala hawana ruhusa ya kujifunza isipokuwa nyumbani kwao kwa waume zao. Biblia inasema kwamba: "Wanawake na wanyamaze katika kanisa maana hawana ruhusa kunena bali watii kama vile inenavyo Torati nayo. Nao wakitaka kujifunza neno lolote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao, maana ni aibu

wanawake kunena katika kanisa." (1 Wakorintho 14:34-35).

### 4. Mwanamke atengwe

Hedhi, yaani damu ya mwezi ni kawaida ya akina mama. Lakini Biblia inawaita najisi na inaamuru kutengana nao. Biblia inasema kwamba: "Mwanamke yeyote, kama anatokwa na kitu, na kitu chake alichokuwa nacho mwilini mwake ni damu, ataketi katika kutengwa kwake muda wa siku saba na mtu yeyote atakaye mgusa atakuwa najisi hata jioni," (Mambo ya Walawi 15:19).

Hii ni hali ya fedheha ya wanawake sawa na Biblia. Hatuwezi kufanya chochote isipokuwa kuwapa pole na kuwakaribisha kwenye ISLAM. Kwani ISLAM ndiyo dini inayokubali haki za watu wote na inawaheshimu. Kwa hiyo Islam ndiyo dini ya watu wote. Karibuni sana.

## MAREJEO MBALIMBALI

Baadhi ya wakati, Wakristo wengine wanapatikana ambao wanapinga taratibu za dini ya Kiislam. Wanakuwa na shauku ya kupinga waila hawajui masikini mafundisho ya dini ya Kiislam wala hawajapata nafasi ya kusoma Biblia. Kama wangesoma Biblia tu, hawangeweza kuonesha tabia ile. Kama vile wanavyopinga udhu wa Kiislam, wengine wanacheka kuwaona Waislamu wakisujudu. Hata juzi juzi Padri mmoja amelalamika juu ya kuvua viatu wakati wa ibada.

Vilevile wanashangaa wakati Waislamu hawaimbi wala hawachanganyiki na wanawake wala hawatumii pombe na nguruwe.

Kama ndugu Wakristo wangesoma tu Biblia wangekuta mafundisho haya yote yanapatikana humo. Kwa kufupisha somo ninaandika hapa mambo ambayo yanaonekana mageni kwa Wakristo ilhali yamo katika Biblia.

### Udhu

Bwana akanena na Musa na kumwambia fanya na birika la shaba, na tako lake la shaba ili kuogea, nawe utaliweka kati ya hema ya kukutania na madhabahu nawe utalitia maji. Na Haruni na mwanawe wataosha mikono yao na miguu yao humo hapo waingiapo ndani ya hema ya kukutania, watajiosha majini ili wasife au hapo watakapoikaribia madhabahu ili watumike

kumteketezea Bwana sadaka ya moto basi wataosha mikono yao na miguu yao ili kwamba wasife na neno hili litakua amri kwao milele kwake yeye na kwa wazao wake katika vizazi vyote.
(Kutoka 30:17-21).

Basi kulikuwako huko mabalasi sita ya mawe nayo yamewekwa huko kwa desturi ya Wayahudi ya kutawadha. Kila moja lapata kadiri ya nzio mbili tatu.
(Yohana 2:6).

**<u>Kuvua viatu wakati wa ibada</u>**

Huyo Amiri wa jeshi la Bwana akamwambia Yoshua, vua viatu vyako miguuni mwako kwa kuwa mahali hapo usimamapo ni patakatifu, Yoshua akafanya hivyo. (Yoshua 5:15).

Naye akasema usikaribie hapa, vua viatu vyako miguuni mwako maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu. (Kutoka 3:5).

**<u>Ibada na Sajda</u>**

Naye Ezra Kuhani akasimama juu ya mimbari ya mti waliyokuwa wameifanya kwa kusudi hilo na karibu naye akasimama Matithia ....... Ezra akakifungua kitabu machoni pa watu wote (maana alikuwa juu ya wote) na hapo alipokijua, watu wote walisimama Ezra akamhimidia Bwana, Mungu Mkuu. Nao wote wakaitika

Amina, Amina, pamoja na kuinua mikono yao kisha wakainama vichwa vyao wakamsujudia Bwana vifudifudi. (Nehemia 8:4-12; Mwanzo 17:3).
Akaendelea mbele kidogo akaanguka kifulifuli akaomba ... (Mathayo 26;39).
Msujudie Mungu. (Ufunuo 22:9).
Musa akafanya haraka akainamisha kichwa chake hata nchi, akasujudu.
(Kutoka 34:8; 1 Wakorintho 14:25).

## **Nyimbo Hazitakiwi**

Niondoleeni kelele za nyimbo zenu; kwa maana sitaki kuzisikia sauti za vinanda vyenu. (Amosi 5:23).
Ninyi mnaoimba nyimbo za upuzi pamoja na sauti ya vinanda na kujifanyizia vinanda vya namna nyingi kama vile Daudi. (Amosi 6:5).

Tena nyimbo za hekaluni zitakuwa vilio siku ile, asema Bwana Mungu. Mizoga itakuwa mingi kila mahali wataitupa wakinyamaza kimya. (Amosi 8:3).

## **Masanamu hayatakiwi**

Usiwe na miungu mingine ila mimi.
Usijifanyie sanamu ya kuchonga, mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, au kilicho chini duniani, au kilicho majini chini ya nchi. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu, (Kumb. 5:7-9).

**Wanawake na wanaume wasichanganyike kwa maombolezi (ibada)**

Nayo nchi itaomboleza kila jamaa peke yake; jamaa wa nyumba ya Daudi peke yao, na wake zao peke yao; jamaa wa nyumba ya Nathani peke yao na wake zao peke yao; jamaa wa nyumba ya Lawi peke yao na wake zao peke yao; jamaa wa nyumba ya Shimri peke yao na wake zao peke yao. Jamaa zote zilizosalia, kila jamaa peke yao na wake zao peke yao. (Zakaria 12:12-14).

**Biblia inaruhusu mitala (wake wengi)**

1. Akiwa mtu ana wake wawili, mmoja ampenda, mmoja hampendi .... (Kumb. 21:15-17).
2. Nabii Ibrahim alikuwa na wake wawili (Mwanzo 16:1-4).

3. Nabii Daud alikuwa na wake wengi na masuria (2 Samuel 12:8 na 15:16).
4. Nabii Suleiman alikuwa na wake mia saba na masuria mia tatu. (1 Wafalme 11:3).

**Kuoga Janaba**

Na mtu yeyote akitokwa na shahawa yake, ndipo ataoga mwili wake wote majini, naye atakuwa najisi hata jioni. Na kila nguo na kila ngozi, ambayo ina shahawa itafuliwa kwa maji itakuwa najisi hata jioni.

Huyo mwanamke naye ambaye mtu mume amelala naye kwa shahawa, wote wawili wataoga majini, nao watakuwa najisi hata jioni.
(Mambo ya Walawi 15:16-18).

**Nguruwe ni haramu**

Naye nguruwe kwa sababu yeye anazo kwato, ni mwenye miguu iliyopasuka kati lakini hacheui, yeye ni najisi kwenu. Msile nyama yao, wala msiiguse mizoga yao, hao ni najisi kwenu.
(Mambo ya Walawi 11:7-8).

Waketio kati ya makaburi, na kulala katika mahali pao pa siri, walao nyama ya nguruwe, na mchuzi wa vitu vinichukizavyo u katika vyombo vyao.
(Isaya 65:4). (Kumb. 14:8).

**Pombe ni haramu**

Usiitazame mvinyo iwapo ni nyekundu, litiapo bilauri rangi yake ishukapo taratibu; mwisho wake huuma kama nyoka; Huchoma kama fira. Macho yako yatakuwa mambo mageni; na moyo wako utatoa yaliyopotoka, Naam, utakuwa kama alalaye katikati ya bahari; Au kama yeye asinziaye juu ya mlingoti. Utasema, wamenichapa wala sikuumia, wamenipiga wala sina habari, Nitaamka lini, nitazidi kuitafuta tena.
(Mithali 23:31-35).
Wote ni mbwa walio bubu, hawawezi kulia, huota ndoto,

hulala, hupenda usingizi. Naam, mbwa hao wana choyo sana, hawashibi kamwe; na hao ni wachungaji wasioweza kufahamu neno, wote pia wamegeuka upande, wazifuate njia zao wenyewe kila mmoja kwa faida yake toka pande zote. Husema, njooni nitaleta divai, na tunywe sana kileo na kesho itakuwa kama leo sikukuu kupita kiasi.
(Isaya 56:10-12).
Ole wao waamkao asubuhi na mapema, wapate kufuata kileo, wakishinda sana hata usiku wa manane mpaka mvinyo imewaka kama moto ndani yao! Na kinubi, na zeze na matari na filimbi, na mvinyo zote ziko katika karamu zao lakini hawaangalii kazi ya Bwana wala kuyafikiri matendo ya mikono yake. (Isaya 5:11-12).

Ole wao walio hodari kunywa kileo chenye nguvu, watu waume wenye nguvu huchanganya vileo, wampao haki mwenye uovu ili wapewe ijara na kumwondolea mwenye haki haki yake.
(Isaya 5;22-23).

Ole wa taji ya kiburi ya walevi wa Efraim na ua la uzuri wa fahari yake linalonyauka, lililo kichwani mwa bonde linalostawi la hao walioshindwa na divai! (Isaya 28:1).

Uzinzi na divai, na divai mpya huondoa fahamu za wanadamu (Hosea 4:11).

**Saumu**

Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. (Mathayo 4:2).

Lakini namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga. (Mathayo 17:21).

**Kutahiriwa**

Siku ya nane mtoto atatahiriwa govi la zunga lake. (Mambo ya Walawi 12:3).

Mungu akamwambia Ibrahimu, nawe ulishike agano langu wewe na uzao wako kwa vizazi vyao baada yako. Hili ndilo agano langu utakalolishika, kati ya mimi na wewe na uzao wako baada yako kila mwanamume wa kwenu atatahiriwa.
Mtatahiriwa nyama ya magovi yenu na jambo hilo litakuwa ishara ya agano kati ya mimi nanyi. (Mwanzo 17:9-11).

Ibrahim mwenyewe alitahiriwa tena katika umri wa miaka 99. Na Ismail pia alitahiriwa siku hiyo hiyo. (Mwanzo 17:24-27).
Yohana alitahiriwa baada ya siku 8. (Luka 1:59).
Yesu pia alitahiriwa baada ya siku 8. (Luka 2:21).
Paulo mwenyewe alitahiriwa. (Wafilipi 3:5).
Paulo ndiye ambaye alifundisha kinyume cha agano hilo kati ya Mungu na Ibrahimu. (Wagalatia 5:2-6).

**Yesu hakuzaliwa Disemba 25**

Hata ikawa katika mwaka wa thelathini na saba wa kuhamishwa kwake Yehoyakini, mfalme wa Yuda, katika mwezi wa kumi na mbili, siku ya ishirini na tano ya mwezi wa Evil - Merodaki mfalme wa Babeli, katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake, akamwinua kichwa chake Yehoyakini mfalme wa Yuda akamtoa gerezani. (Yeremia 52:31).

**Idi pia yapatikana katika Biblia**

Mtafanya nini katika siku ya mkutano wa Idi; na katika siku ya karamu ya Bwana? (Hosea 9:5).

**Waanzilishi wa Ukristo ni Paulo na Barnabas.**

Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia (Matendo 11:26).

**Harusi ya Kaini.**

Kaini akatoka mbele ya uso wa Bwana akakaa katika nchi ya Nodi mbele ya Adeni. Kaini akamjua mkewe naye akapata mimba akamzaa Enoko naye akajenga mji akauita Henoko kwa jina la mwanawe.
(Mwanzo 4:16-17)

**Kukumbuka kwa urahisi**

1. Yesu hakufufuka. (1Wakorintho 15;15).
2. Mwandishi wa Mathayo si Mathayo. (Mat. 9:9).
3. Wanawake na wanaume wasichanganyike (Zakaria 12:12).
4. Nabii mfano wa Musa atakuja. (Kumb. 18:18).
5. Taurati iwe uwongo. (Yer. 8:8).
6. Ismail akakaa katika jangwa la Paran na mama yake. (Mwanzo 21:21).
7. Naye Ibrahimu alikuwa mtu wa miaka 86, hapo Hajira alipomzalia Ibrahimu Ismail. (Mwanzo 16:16).
8. Wale wanaomwita Yesu Bwana Bwana na wanatoa mapepo kwa jina lake watafukuzwa siku ya Kiyama. (Mat. 7:22-23).
9. Waacheni wafu wazike wafu wenzao. (Mat. 8:22).
10. (Yesu alisema) Wote walionitangulia ni wevi na wanyang'anyi. (Yohana 10:8)
11. Yesu aliwaambia amani iwe kwenu (yaani Assalaamu Alaikum). (Yohana 20:19).
12. Yesu alikuwa akienda sinagogi. (Luka 4:16). Sinagogi ni msikiti (maelezo ya maneno).
13. Msimwambie yeyote kwamba mimi ni Kristo. (Mat:16:20).
14. Kwa sababu ya upungufu wa imani yenu. (Mat. 17:20).
15. Sanamu zao ni fedha na dhahabu kazi ya mikono ya wanadamu, zina vinywa lakini hazisemi, zina macho lakini hazioni, zina masikio lakini hazisikii, zina pua lakini hazisikii harufu, zina mikono lakini hazishiki, zina

miguu lakini haziendi wala hazitoi sauti kwa koo zake. (Zaburi 115:4-7).
Je, sanamu za Mariamu na Yesu hazipatikani makanisani?

**Maswali Kwa Wakristo**

Hapa chini ninaandika baadhi ya maswali kwa ajili kuwauliza mapadri na ndugu Wakristo, ili watusaidie majibu sawa na Bibilia.

1. Katika aya gani ya Biblia Mwenyezi Mungu amesema kwamba Yesu ni Mungu?
2. Katika aya gani ya Injili Bwana Yesu amedai kuwa yeye ni Mungu?
3. Kama Yesu ni Mwana wa Mungu, basi Mungu na Mariamu (Mama wa Yesu), wanao uhusiano gani baina yao. Maana Mungu hawezi kupata mtoto bila ya mke, basi mke wa Mungu ni nani?
"Inamkinikaje awe na mwana hali hana mke (Qur'an 6:102).
4. Biblia inasema: Akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti, ili litimie neno lililonenwa na manabii, ataitwa Mnazarayo. (Mat: 2:23).
Hawa manabii ni akina nani na walinena wapi?.
Ushahidi wa kitabu unahitajika.
5. Je unakubali kwamba Yesu ni mwizi? Kwa sababu mwenyewe amesema kwamba ujaji wake wa mara ya pili utakuwa sawa na ujaji wa mwizi. (Mat 24:43; Ufunuo 3:3 na Petro 3:10).

**Iwapo unapenda kununua vitabu zaidi vya Dini ya Kiislamu au kwa maelezo zaidi ya mafundisho ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, wasiliana na anuani iliyo karibu nawe kati ya hizi zifuatazo:**

1. P. O. Box 376, Simu: 2110473 Dar es Salaam.
2. P. O. Box 1, Simu: 2603477 Morogoro.
3. P. O. Box 260, Simu: 2646849 Tanga.
4. P. O. Box 359 Iringa. Simu 2700633.
5. P. O. Box 196, Simu: 243043 Dodoma.
6. P. O. Box 94, Simu: 2600847 Songea.
7. P. O. Box 10723 Arusha.
8. P. O. Box 54, Simu: 2603291 Tabora.
9. P. O. Box 547 Ujiji - Kigoma.
10. P. O. Box 306, Simu: 2333919 Mtwara.
11. P. O. Box 86, Simu: 2510082 - Masasi.
12. P. O. Box 1812 Bukoba.
13. P. O. Box 28, Simu 70 Kibiti - Rufiji.
14. P. O. Box 391 Tarime.
15. P. O. Box 605 Ifakara.
16. P. O. Box 17 Kilosa.
17. P. O. Box 40554, Simu: 764226 Nairobi Kenya.
18. P. O. Box 97011, Simu: 492624 Mombasa Kenya.
19. P. O. Box 421, Simu 40269 Kisumu Kenya.
20. P. O. Box 77, Simu 52 Shianda Kenya.
21. P. O. Box 552 Limbe Malawi.